CHUO CHA BIBLIA

VITABU VYA
WAEBRANIA, YAKOBO, 1&11 PETRO, 1,11 &111 YOHANA, YUDA, NA UFUNUO WA YOHANA.

KITABU CHA 15

SURA YA KWANZA
Waraka Wa Waebrania.

Tayari tumemaliza nyaraka za mtume Paulo kwa vikundi maalumu na sasa kunakaribia nyaraka za jumla, ambazo zinafahamika hivyo kwa sababu ziliandikwa kwa umma. Tunaanza na waraka kwa Waebrania. Hatujui ni nani aliyeandika waraka huu. Imedaiwa kwamba ni Paulo, lakini neno la kwanza katika kitabu hiki sio 'Paulo' jinsi ilivyo katika nyaraka zake. Kuna sababu nyingi nzuri kwa nini wasomi hawaamini kuwa Paulo ndiye aliyeandika kitabu hiki cha Waebrania.

Jinsi tayari tumeona katika uchunguzi wetu wa Biblia, jambo la muhimu kuhusu kitabu cho chote ni: 'Je kitabu chenyewe kinasema nini?' 'Kinamaanisha nini?' Na 'hayo yanamaanisha nini kwangu?' Jambo la muhimu kuhusu kitabu cha Waebrania ni ukweli ambao unazungumziwa ndani yake na matumizi ya kibinafsi ya ukweli huo katika maisha yangu na yako.

Ye yote aliyeandika kitabu hiki alikuwa msomi mwenye ufasaha ambaye alielewa kile agano zote zilivyokuwa zikisema kuhusu Yesu Kristo. Mchango wa kitabu hiki ni zaidi ya vitabu vile vingine katika Biblia, kwani kinaunganisha pamoja agano zote. Je, umewahi kushangaa kwa nini hatutoi sadaka za wanyama kwa ajili ya dhambi zetu? Basi kitabu hiki kina majibu kwa swali hilo sawa na maswali mengine.

Hoja Ya Kitabu Cha Waebarania.

Unaposoma kitabu hiki cha Waebrania, utatambua kuwa ni hoja inayowasilishwa pamoja na elimu ya kuwazia kuanzia aya ya mwanzo hadi ya mwisho. Jaribu kufuatilia elimu hiyo ya mwandishi unaposoma kitabu hiki. Jaribu kusoma kitabu hiki kwa kikao kimola ikiwa unaweza kufanya hivyo. Unaposoma, tafuta hoja yake, tambua kuwa kuna maneno matatu ambayo yanaweza kukuongoza. Neno la kwanza ni 'bora,' ilhali la pili ni , 'amini' huku la tatu likiwa ni 'jiadhari.'

Mwandishi wa kitabu hiki anawaandikia Waebrania huku akitaka wafahamu kuwa Yesu Kristo ni bora kuliko mambo yote ambayo wanaheshimu. Anaandika hivi**,** *'Mnawatendea wema manabii lakini Yesu Kristo ni bora kuliko manabii. Yesu ni nabii. Mungu alizungumza kupitia manabii lakini sasa anazungumza kupitia Mwanawe. Mwanawe ni bora kuliko manabii wote.'*

Katika sura zake za mwanzo mbili za kitabu hiki, mwandishi anasema kuwa Yesu Kristo ni bora kuliko malaika. Wayahudi walikuwa ni wafuasi wa mambo na desturi za kale, pamoja na imani halisi, sawa na Mafarisayo, walioamini malaika.

Wayahudi pia walimheshimu sana Musa, kwa hivyo mwandishi huyu anaandika kuwa Yesu Kristo pia ni bora kuliko Musa. Mwandishi anatutupa picha ya neno hili: Nyumba ina thamani, lakini mjenzi wa nyumba ana thamani zaidi kuliko nyumba yenyewe. Musa alijenga nyumba, yaani taifa la Waebrania, lakini ni Yesu Kristo Mwana wa Mungu anayeishi ndani ya nyumba hiyo.

Kisha mwandishi huyu anawasilisha hoja nyingine kuwa Yesu Kristo ni bora kuliko Yoshua; ambaye aliwaongoza wana wa Israeli hadi nchi ya ahadi na

kuwapumzisha. Hata hivyo, Yesu aliwapa pumziko ambayo inazidi hiyo waliyopokea wakati walipoingia nchi ya ahadi.

Kisha anasema kuwa Yesu Kristo ni bora kuliko makuhani wote. Wayahudi hao walikuwa na stahi kuu kwa Wayahudi. Kuanzia sura ya tano, anasema kuwa Yesu Kristo ni bora kuliko makuhani hao.

Baada ya makuhani, anazungumzia juu ya agano. Kulikuwa na ahadi ya Nuhu, Ibrahimu, Musa na Daudi. Mungu alifanya ahadi nyingi, lakini mwandishi wa kitabu hiki anasema kuwa Yesu ni bora kuliko ahadi hizo zote.

Mwishowe, anazungumzia juu ya hema ya kuabudia huku nyikani. Unaweza kukumbuka kuwa hekalu la Sulemani lilijengwa kwa mtindo sawa na hema hilo la kuabudia waliyokuwa wakitumia wakati huo walipokuwa huko jangwani. Sawa na matarajio yetu, mwandishi huyu anasema kuwa Yesu Kristo ni bora kuliko hema la kuabudia. Anawaambia waumini Wayahudi kuwa, *'sikizeni enyi, hema la kuabudia, hekalu na Sulemani, na mitindo yote ya kuabudu ambayo ilikuwepo, ilikuwa tu nakala, za mambo yaliyo mbinguni kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyika kwa mikono* (***Waebrania 9: 11, 23-26).'***

Mara moja kwa mwaka, kuhani mkuu alikuwa akiiingia ndani ya hema hilo pahali ambalo palikuwa panajulikana kama 'patakatifu pa patakatifu.' Angepeleka huko sadaka ya damu ambayo aliitoa kwa ajili ya dhambi za watu wote. Haya yote yalikuwa mitindo ya yale yatakayotokea huko mbinguni baada ya Yesu Kristo kufa juu ya msalaba. Ilikuwa kana kwamba, vile Kuhani mkuu alivyoingia huko ndani kwa ajili ya dhambi za dunia yote, Yesu alifanya hivyo kupitia damu yake ya thamani. Sadaka yake ilitimiza na kuthibitisha sadaka hizo zote ambazo zilitolewa kwa Mungu kupitia makuhani na taratibu zote zilizoandamana na sadaka ambazo zilikuwepo tangu nyakati za Musa hadi Yesu. Mwandishi huyu anaunganisha nyaraka mbili anapoandika kuwa baada ya Yesu kufa msalaani, hatupaswi tena kutoa sadaka kwa ajili ya dhambi zetu.

SURA YA PILI
Ni Bora Uliamini!

Maneno yale mengine mawili ni 'amini' na 'jiadhari.' Mwandishi anatupatia onyo nyingi kuhusu hila za ukafiri-akichukua msimamo wa hoja moja katika safari yako ya imani, kisha baadaye msimamo mwingine kando na ule wa zamani. Dhana yake ya ukafiri sio nyingi kama ya mtu ambaye ana thiolojia mbaya, bali ni mtu aliye na nzuri ambalo alifanyii cho chote.

Kitabu hiki kimejaa mashauri na onyo. Neno lingine ambalo mara kwa mara linaandamana na onyo ni 'isiwe', ambalo pia linaezwa kama –'ili' au 'iwapo' ***(Waebrania 2:1, 3:13, 4:1, 11).*** Nyingi za onyo zinahusu kazi ya Kristo ndani yetu, au pamoja na kazi ya Kristo kupitia sisi. Ushauri katika kitabu hiki unafuata neno 'na tu...'***(Waebrania 4:1. 11, 10:22, 23, 24).***

Unaposoma kitabu cha Waebrania, jaribu kutazamia hoja ya kitabu chenyewe. Unapoelewa hoja hiyo, pia utakuwa umeelewa nia ya kitabu chenyewe, ambayo ni kuwatia moyo waumini wa asili ya Waebrania waliokuwa wanateseka, bila matumaini kiasi cha kutupilia mbali imani yao. Nia yake ilikuwa kuwatia moyo watu hao ambao bado hawakuwa na imani ndani ya Yesu. Alipokuwa akiwazungumzia hao waliokuwa

bado kuingia katika imani halisi; ni wazi kuwa alitaka kuwavua hakikisho la uongo kutoka kwa hao ambao bado hawakuwa wamefanya agano halisi ya imani yao.

Onyo za mwandishi zinaendelea anapotazamia katika historia ya Waebrania ambayo imerekodiwa katika sura ya kumi na nne ya kitabu cha Hesabu. Wakati wana wa Israeli walipokuwa wakitaabika huko jangwani kwa muda wa miaka arobaini, kwa mara kumi Mungu aliwapa changa moto kuumwamini kupitia kufanya miujiza. Alikuwa akijaribu kuwapa imani na ujasiri wa kuvamia miji iliyokuwa imara ya Kanaani.

Mungu alifikia kiwango ambapo aliwaambia wana wa Israeli, '*nimechoka nanyi. Hamtaingia nchi ya ahadi. Watakaoingia huko kati yenu ni Yoshua na Kalebu kwa sababu wameniamini.'* Mwandishi wa kitabu hiki anawaonya kutowaiga mababu zao kwani walikosa imani, bali kuingia katika nchi yao ya ahadi, ambayo najulikana kama 'raha.***' *(Waebrania 3:7-4:1).***

Kwenye sura ya tatu na ya nne, mwandishi anaandika hivi: *Basi, ikiwa unasikia sauti ya Mungu lakini halisikilizi, basi wewe ni sawa na watu hao waliokuwa huko jangawani ambao walizunguka huko kwa miaka arobaini. Siku inakuja ambapo hutasikia sauti ya Mungu tena. Mungu atageuka bali nawe na hautaingia katika Nchi ya Ahadi ambayo ina uzima tema ndani ya Kristo kwa sababu sauti itafififia na kufifia.'*

Katika sura ya tano, mwandishi atazungumzia swala ambalo ni ngumu sana kuelewa. Yuko karibu kuonyesha jinsi Yesu Kristo alivyo bora kuliko makuhani wote. Wayahudi wangetarajia mwandishi huyu kuwaonyesha kuwa Yesu alikuwa kuhani mfano wa Haruni na na Levi. Kuanzia mwanzo wa mazungumzo yake, anataka kuwasilisha hoja kuwa Yesu ni kuhani maalumu mfano wa Melkizedeki.
Kwa wakati huo, anawasilisha hoja anapoandika kuwa, '*Ambaye tuna maneno mengi ya kunena katika habari zake; na ni shida kuyaeleza kwa kuwa mmekuwa wavivu wa kusikia.'* Katika hoja hili, anaelezea hali kuwa hawana ufahamu wa Maandiko kiasi kuwa wangeweza kuelewa kile anachotaka kuwaeleza kuhusu Melkizedeki. Anaelezea aina ya vyakula vya kiroho ambavyo wanahitaji ili kukua kiroho ***(Waebrania 5: 11-14).***

Unaponenda Kanisa, mchungaji wako ambaye amekula baadhi ya vyakula vya kiroho katika Maandiko, huwa anakufunza yale ambayo tayari amekula. Hayo ni sawa na kunywa maziwa, ambayo tayari yameyeyushwa kwa ajili ya watoto wadogo ambao bado hawajaimarika. Ikiwa Maandiko yale tu unayofahamu yanakuja kwako kupitia mchungaji ambaye tayari ameyayeyusha, basi hali hiyo inakufanya kuwa mtoto kiroho.

Hata hivyo, ikiwa unakaribia Maandiko peke yako, ukiwa na Roho Mtakatifu na Biblia, basi Roho huyo atakufunza Maandiko hayo, na utakuwa unakula nyama ya kiroho kwa ajili ya kuimarika kiroho.

Kulingana na mtume Yohana, kutokana na kuzaliwa mara ya pili, Kristo amekuja kuishi ndani ya moyo wako. Umepokea 'upako' kutoka kwa Roho Mtakatifu. Yohana anataka utambue kuwa, *'nanyi, mafuta yale mliyopata kwake yanakaa ndani yenu, wala hamna haja ya mtu kuwafundisha; lakini kama mafuta yake yanavyowafundisha habari za mambo yote, tena ni kweli wala si uongo, na kama yalivyowafundisha, kaeni ndani yake* (***1Yohana 2:2-27)'***

Nayo sura ya sita ya kitabu hiki cha Waebrania ina baadhi ya aya ambazo zimechokoza nafsi zilizojitolea kwa karne nyingi (***Webrania 6: 4-12).*** Baadhi ya watu wanaamini kuwa kifungu hiki kinafunza kuwa, sisi kama waumini wa kweli tunaweza kupoteza wokovu wetu. Sikuibaliani nao. Mwandishi anaandika hivi, *'lakini, wapenzi, ijapokuwa twanena hayo, katika habari zenu tumesadiki mambo yaliyo mazuri zaidi, na*

yaliyo na wokovu.' Anapoandika kuhusu kusadiki, kuoja, na kushiriki, hasimulii juu ya muumini ambaye ameshuhudia 'kuzaliwa mara ya pili.' Bali anaelezea kuhusu mtu ambaye amevutiwa na Roho Mtakatifu kiasi kuwa anaoja, au kushiriki, ingawa bado hajavuka mstari wa imani na kuzaliwa upya.

Nakukumbusha kuwa moja ya nia za kitabu hiki ni kuwashauri Wayahudi, ambao bado hawajamwamini Yesu Kristo, kufanya ahadi kuu ya imani ndani Yake. Kusudi la hoja ya kitabu hiki ni kuwapa changa moto kusimama na kufanya ahadi halisi kwa Masihi wao, kisha kuhakikishiwa wokovu. Naamini kuwa hiyo ndio nia ya ujumbe wa ushauri huu mgumu katika sura hii ya sita ya waraka kwa Waebrania.

Sura ya sita, aya ya nne hadi ya sita, inapaswa kutafsiriwa katika misingi ya hoja kuu na huduma ya kitabu hii. Kulingana na mwandishi, hazungumzii mambo ambayo yanaandamana na wokovu. Ushauri wake kote katika kitabu unaelekezwa kwa waumini ambao bado hawajazaliwa mara ya pili kwa sababu wana upunguvu wa imani katika kujitoleoa kwao kwa Yesu. Mwandishi anawaonya watu hao kuwa wao ni sawa na wale wanaoenda sokoni na kutazama-kutazama na kutazama, lakini hawanunui cho chote. Onyo lake hapa katika kifungu hiki ni kuwa, yai hufikia kiwango ambapo linaangua au linaonza.

Kufafanua mfano huu wa Yesu, kile mwandishi wa kitabu hiki cha Waebrania anachotaka wasomi wake kuwa, ni wao wawe wamezaliwa mara ya pili. Hoja yake katika kifungu hiki kigumu sana ni kuwa punde wanapozaliwa mara ya pili, hawatapoteza wokovu wao. Lakini kabla ya kizazi hicho kipya kufanyika, kunaweza kuwa na 'kuharibika mimba' kwa kiroho. Wao wako katika hatari ya 'kuavywa' bado wakiwa katika kipindi hicho cha 'kuchukua mimba' kiroho.

SURA YA TATU
Mtazamo Wa Imani.

Kiini cha ujumbe huu kinapatikana katika sura ya kumi na moja ya kitabu chenyewe. Sura hii ya kumi na moja inajulikana kama 'sura ya imani' ya Biblia. Sura yenyewe hakika inaanza hapo mwisho wa sura ya kumi wakati anapoanza kuwapa wasomi wake sababu za kutotupilia mbali imani yao (***Waebrania 10:35).*** Anaandika kuwa hawapaswi kutupilia mbali imani yao kwa sababu imani iliwaokoa. Anawashauri kufikiria tena wakati ule walipoamini mara ya kwanza kisha wakaokolewa. Huu ndio uaminifu wa hoja-usitupe imani yako kwa sababu hiyo ndio iliyokuokoa!

Kadiri ilivyo, walikuwa wameshuudia kubadilishwa halisi kwa Kristo ambako kuliandamana na upendo wa kwanza kwa Kristo. Anawakumbusha kuhusu ushuhuda, jinsi walistahimili kupoteza mali yote, wakifahamu kuwa huko mbinguni walikuwa na thawabu kuu. Sasa, mwandishi anasema, *'fikiri tena wakati huo wa imani na kuokolewa kwako kisha ufikirie maana yake kwako. Tambua kuwa uliokolewa kwa sababu ya imani yako. Kwa hivyo, cho chote ufanyacho, usitupe imani yako iliyokuokoa.'*

Kisha, kwenye aya ya thelathini na nane ya sura ya kumi, anamnukuu nabii Habakuki, *'Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa amani **(Habakuki 2:4).**'* Katika maandiko haya, anaandika kuwa: *'huwezi kutupa imani yako kwa sababu unalihitaji. Umeokolewa tu kwa imani; ni lazima ushi kwa imani.'*

Imani ni ngumu sana kuelezea, ingawa hata hivyo unaweza kujaribu kulielezea. Anaandika kuwa: *Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana na mambo yasiyoonekana.'* Tumaini ni kusadiki kuwa jambo nzuri liko hapa duniani na kuwa siku moja utalipata. Waumini wa agano la kale walizungumzia kuona mema. Daudi aliwapa *changa moto walioshidwa na watoto kwa swali hili: 'Ni nani mtu yule apendezwaye na uzima?'* Kisha alijibu swali hilo mwenyewe kwa kutoa mwaliko huu: *'Onjeni mwone ya kuwa Bwana yu mwema; heri mtu yule anayemtumaini!* ***(Zaburi 34:12, 8).'*** Kwa imani, lazima kuwe na thibitisho la kuimarisha kusadiki kuwa jambo nzuri litaenda kufanyika.

Lakini hapa, yaliyomo ya hoja hili ni, 'usitupe imani yako kwa sababu ya maana yake. Imani ni kuwa na hakika ya tumaini au msingi ambao unafanya tumaini lako kuaminika. Imani ni thibitisho la mambo yasiyoonekana, ambayo ni, vyombo visivyoonekana vya imani yako.

Wakati imani yako inapokuwa ya Kibiblia, vyombo au vifaa vya imani hiyo vinapaswa kuwa visivyoonekana. Unaondoa hoja ya imani unapoona vifaa vyenyewe. Ikiwa imani yako ni ya kiroho, basi vifaa vyake havionekani, lakini kuna thibitisho ambalo linaunga mkono kusadiki kuwa vyombo hivyo visivyoonekana viko. Kuna harufu ya chakula tamu ambacho bado haujakiona, lakini harufu yenyewe linkuhakikishia kuwa kiko tayari kupakuliwa. Kwa hivyo, maelezo mwafaka ya imani yanapaswa kuwa: 'Imani ni kitendo cha kuamini jambo, au mtu, ambaye huwezi kumwoma, ambacho kinahusika na thibitisho.'

Kwa hali hii, chombo kisichoonekana ni Mungu. Na mwandishi anasema kuwa thibitisho kuu hapa duniani kuwa kuna Mungu ni mtu aliye na imani. Kulingana na agano jipya, imani ni karama ya Mungu. ***(Waefeso 2:8' Wafilipi 1:29).*** Kwa hivyo, aliye na imani ndiye thibitisho kuu hapa duniani kuwa Anayepeana imani yuko. Anaandika hivi: 'Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana na mambo yasiyoonekana.' Kati na mambo yale mengine, mwandishi wa ujumbe huu anatueleza kuwa imani, ni bayana inayoelezea kuwepo kwa Mungu asiyeonekana.

Anawasilisha kwa wasomi wake sababu nyingine kwa nini hawapaswi kutupilia mbali imani yetu kwa kuwaandika hivi: *'Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba Yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamfuatao* (***Waebrania 11:6).'***

Anashikilia sababu hiyo, kwa nini imani haipaswi kutupiliwa. Anawasilisha hoja kuwa hawapaswi kutupa imani yao kwa sababu bika imani, hawawezi kumwona Mungu, au kumpendeza. Kisha anawaambia (pamoja nasi) juu ya watu waliompendeza Mungu kwa sababu walikuwa na imani.

Henoko alihamishwa kwa sababu ya amani yake. Ni kana kwamba Henoko alienenda karibu na Mungu hivyo siku moja Mungu akamwambia, 'Henoko, tumekuwa karibu sana kwa nyumba yangu kuliko nyumba yako; kwa nini usikuje na kuwa pamoja nami?' Mungu alimchukua Henoko hadi mbinguni kwa sababu mtu huyu alienenda pamoja naye na kumpendeza ***(Waebrania 11:5).***

Kisha, anawapa mifano wa watu wa Mungu waliokuwa na imani. Soma kitabu chetu cha Waebrania kupitia sura ya kumi na moja, kisha upige mstari viarifa vyote, yaani maneno ya matendo. Wote walikuwa mashujaa wa imani kwa sababu walitenda jambo. Hii ndio sababu imani ni kitendo cha kuamini katika mtu fulani, au jambo fulani, ambalo huwezi kuliona, ambalo ni hakika ya mambo yatarajiwayo.

Wakati Mungu alipoamuru Nuhu kujenga safina, hakukuwa na mvua duniani. Mwandishi anaelezea changa moto kwa imani ya Nuhu kama, 'Mambo yasiyoonekana.' Nuhu hajawahi kuona mvua. Hadithi ya Nuhu, ambalo linaendelea katika sura nne za kitabu cha Mwanzo, imesimuliwa kwa aya moja katika sura ya imani yaani: *'kwa imani, Nuhu akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasiyoonekana bado kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake. Na hivyo akahukumu makosa ulimwengu, kwa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani **(17).'***

Nuhu alikuwa mhubiri wa haki wakati huo wa kipidi cha miaka mia moja ishirini alipokuwa akijenga safina. Njia ile ungeokolewa ni kuwa ndani ya safina hilo. Petro anatueleza kuwa safina ni picha ya wokovu. Katika sura hii, tunajulishwa kuwa Nuhu ni picha ya imani na maana pamoja na kile imani hiyo inachoweza kufanya.

Watu wengi wanaamini mfano mwandishi anaowasilisha katika ***12:1-2*** kuwa sisi tu wana mbio wanaopiga mbio ilhali mashambiki walio kwenye uwanja wakitutazamia ni 'wingu kuu la mashahidi.' Tayari wamepiga mbio zao. Unaamini kuwa inawezekana watu waliokufa, waliokwenda kabla yetu, kujua kile kinachotendea katika maisha yetu leo? Mwandishi huyu wa kitabu cha Waebrania anaweza kuwa anaongezea katika hoja lake hapa katika sura ya imani, kuwa hatupaswi kutupilia mbali imani yetu kwa sababu wingu kuu la mashahidi linatutazama na kutushangilia tunapopiga mbio kwenye uwanja.

Wewe ni mwana mtoto wa Mungu na kwa sababu hiyo, unapokosa kumtii, naye atakurudi. Kulingana na mwandishi huyu, ukiwa unateseka kwa sababu unatakaswa, basi huwa kuteseka kwako ni thibitisho la kuwa mwana wa Mungu. Anaandika hivi: '*Mwanangu, usiyadharau marudia ya Bwana, Wala usizimie moyo ukikemewa naye; Maana yeye ambaye Bwana ampenda, humrudi, Naye humpiga kila mwana amkubaliye.'* Mwandishi pia anatufahamisha kuwa kurudiwa kunazalisha tunda la haki la amani.

Mwandishi huyu anamalizia ujumbe huu kwa kutushauri kuwa wakarimu. Anaandika katika sura yake ya mwisho kuwa, 'Kisha anatueleza kuwakumbuka *Msisahau kuwafadhili wageni; maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua.'* wafungwa kana kwamba tumefungwa pamoja nasi. Wengi wa washiriki wa Makanisa ya kale walikuwa wafungwa. Mwandishi anatamatisha kwa ushauri wa kutii wachungaji wa kiroho ambao wana jukumu la hali yetu ya kiroho.

SURA YA NNE.
Waraka Wa Yakobo.

Waraka wa Yakobo ni wa matendo, na unajulikana kati ya wengi kama, 'Mithali ya agano jipya.' Ni sawa na maelezo ya Yesu Kristo, hasa mahubiri yake ya Mlimani. Unaweza kupata takribani mifano kumi ambapo mafunzo hayo ya Yesu yalifafanuliwa na kujumulishwa na Yakobo.

Wasomi wengi wanaamini kuwa Yakobo aliyeandika waraka huu alikuwa nduguye halisi wa Yesu Kristo. Hakumwani Yesu wakati Bwana alipokuwa hapa duniani katika hudumu kwa muda wa miaka mitatu. Baada ya kufufuka, tunajulishwa kuwa Yesu alijitokeza kwa Petro na Yakobo, yaani nduguye huyu (***1Wakorintho 15: 7).***

Ni ajabu kutambua kuwa baada ya Yakobo kubadilishwa, alikuwa karibu kuteuliwa kuwa moja wa viongozi wakuu wa Kanisa la agano jipya. Yakobo ndiye

aliyeongoza baraka hilo la Yerusalemu ambalo linazungumziwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume sura ya kumi na tano.

Huyu ndiye Yakobo ambaye mtume Paulo anaelezea katika waraka kwake kwa Wagalatia kuwa alipopanda kuelekea mjini Yerusalemu, kulikuwa na watu watatu ambao walionekana kana vinara katika mji huo-Yoahana, Petro na Yakobo.

Historia inadokeza kuwa Yakobo alitupwa na kuhani mkuu kutoka kwenye kinara cha Kanisa na kufa. Wakati jambo hili lilipotendeka, historia inasema kuwa jamii ya Wayahudi Wakristo waliandama na kuasi dhidi ya kuhani huyo mkuu na kumwondoa kwenye mamlaka. Wakati mtawala wa Warumi, Tito, alipovunja mji wa Yerusalemu mnamo mwaka wa sabini baada ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo, wengi wa asili ya Wayahudi ambao hawakuwa wafuasi wa Yesu, waliamini kuwa ilikuwa hukumu ya Mungu dhidi ya mji huo kwa sababu ya mauaji ya kidini ya mcha Mungu Yakobo.

Kwa kuwa Yakobo ni waraka, unafikia mwisho wa agano jipya pamoja na nakala za jumla. Wengi wa wasomi wa kitabu hiki wanaamini kuwa kitabu chenyewe ndio cha kale kabisa katika agano jipya.

Ujumbe Wa Yakobo

Unaposoma waraka huu, utaona kwa nini baadhi ya watu wanaamini kuwa Yakobo alikuwa akijaribu kuwasilishwa usawa katika mafunzo ya Paulo. Wanatufahamisha kuwa Paulo anajitokeza kwa ujasiri pamoja na hakikisho la imani wala sio kwa matendo. Katika sura ya pili ya waraka huu, Yakobo atatueleza kuwa tunahesabiwa haki sio tu kwa imani bali pia kwa matendo. Ingawa waraka huu unajitokeza hapo mwisho wa agano jipya, nyaraka za Paulo ziliandikwa baada ya waraka huu kuchapishwa. Wasomi wengi wanaamini kuwa Yakobo aliandika kabla ya watu wa mataifa kujiunga na Kanisa. Hii ndio sababu waraka wa Yakobo unaonekana kuwa wa Wayahudi na wenye amri.

Aina Mbili Ya Majaribu

Katika sura ya kwanza ya waraka huu, tunajifunza kuwa Yakobo ni mtu ambaye hausiki sana na mambo halisi (jinsi yalivyo) bali na vyanzo vyake. Yeye ni sawa na Yesu kwa hali hiyo. Yesu alitilia mkazo utu wa ndani na maswala yanayohusika na utu huo. Yesu pia alitilia mkazo tabia yetu kuhusu maneno na nia inayotuongoza kwenye matendo yetu. Maana ya waraka wa Yakobo inaenda sambamba na thamani ambazo Yesu alitilia mkazo katika mafunzo yake.

Katika sura ya kwanza, Yakobo anatufahamisha kuhusu vyanzo na utaratibu wa majaribu yetu. Katika baadhi ya tafsiri, majaribu hayo yanasimuliwa kama tamaa. Atatufautisha baadaye aina hizi mbili za tamaa, ingawa kwa wakati huu anaelezea juu ya majaribu yao ya mateso. Katika maneno yake ya utangulizi, Yakobo anaandika hivi: *'Hesabuni ya kuwa ni furaha tupu'* unaposhuhudia majaribu. Yakobo anatueleza kuwa tunapaswa kushangilia katika majaribu yetu kwa sababu: *'kujaribiwa kwa imani yetu huleta saburi.'* Na ikiwa tunawacha majaribu ya imani kuleta saburi ya imani, basi yutashuhudia ushindi wa imani, ambao Yakobo anataja kama 'taji la uzima.'

Unapokumbwa na mawimbi katika maisha yako, majaribu hayo mara kwa mara yatakuleta mahali ambapo haujui jinsi ya kufanya. Utatambua kuwa unahitaji hekima nyingi. Yakobo anaandika kuwa tunapaswa kuacha majaribu ya imani yetu kutuongoza

katika imani. Tunapokosa hekima, tunapaswa kumwuliza Mungu, ambaye anavutiwa sana kushirikiana nasi hekima Yake.

Elimu Ya Jinsi Dhambi Ilivyo

Yakobo kisha anaelezea aina ya majaribu ambayo hatupaswi kushangalia. Mungu si chanzo cha majaribu ya dhamabi. Katika sehemu ya pili ya sura ya kwanza ya waraka huu, Yakobo anatupa 'elimu ya jinsi dhambi ilivyo.' Anafunza kuwa majaribu hayatokani na muovu. Bali, hutoka katikati mwako na mimi.

Yanafanya kazi hivi: Utaratibu wa kwanza ni, kuna jambo la kuona. Kisha kuna kuvutiwa, au hamu kuu ya kile tayari umeona. Ni kana kwamba kile umeona ni kifaa cha chuma na hamu yako ni sawa na nguvu za simaku. Ikiwa hautafanya jambo kuvunja nguvu hizo za simaku kati ya hamu yako na kifaa hicho unachotamani, siku moja kutakuwa na mgongano wa tamaa.

Kulingana na na Yakobo, tamaa sio dhambi. Bado haujatenda dhambi kwa sababu umevutiwa tu kutenda. Tunafahamishwa kuwa Bwana alijaribiwa sawa nasi katika mambo yote, bila kufanya dhambi (***Waebrania 4: 15).*** Sio dhambo kujaribiwa, lakini majaribu huleta kitendo wazi au dhahiri ya dhambi. Unapotumbukia ndani ya majaribu na hatimaye kufanya dhambi, madhara yake huwa ni mauti (***Warumi 6:23).***

Hoja katika elimu hii ya dhambi ni; ikiwa hautaki kufanya dhambi, basi ni shari ushinde vita dhidi ya dhambi katika mambo yote ya hamu kabla ya kukabilina na tamaa. Yesu alitufunza kuomba kila mara hivi, '*Na usitutie majaribuni* (***Mathayo 6:23).***

Kwa Muhtasari

Katika sura yake ya kwanza, Yakobo anatueleza jinsi Mungu anaweza kutuimarisha kiroho katika majaribu yote. Yakobo pia anasema kuwa kuna maswala mengine, majaribu ya kutenda dhambi. Mungu sio chanzo cha utaratibu wa majaribu ambayo hutela dhambi na hatimaye mauti. Hakuna jambo nzuri kuhusu dhambi. Muhtasari wa sura ya kwanza ya Yakobo unaweza kuwa: Kujaribiwa katika uzima, kujaribiwa katika mauti na kufunza tofauti.

SURA YA TANO
Aina Mbili za Dini.

Yakobo anatufahamisha kuwa Neno la Mungu ni mjumbe au balozi mwenye uvuvio ambaye anaweza kuleta uzima wa kiroho ndani ya moyo wako na kukupa ushuhuda wa kuzaliwa mara nyingine. Kuzaliwa huko kunaweza kukupa nguvu na uwezo wa kuishi juu mbali na dhambi.

Baada ya mafunzo yake katika sura ya kwanza ambapo alishiriki nasi habari ya huzuni kuhusu majaribu na dhambi, Yakobo alishiriki tena nasi habari njema jinsi Mungu anavyofanya miujiza ya wokovu katika mioyo yetu. Yakobo anaandika kuwa Neno la Mungu ni mahali tunapopata suluhisho kwa shida za majaribu na dhambi. Anatupa ushauri mkuu ambao unazidi katika sura ya pili kuhusu umuhimu wa kutii Neno la Mungu. Baada ya kutufahamisha kuwa Neno lililopandwa la Mungu ni mjumbe mwenye uvuvio ambaye huraisisha kuzaliwa kwetu mara ya pili ikiwa tutaitikia vyema, Yakobo anatupatia ushauri mkuu katika hali ya mfano mzuri sana: 'Neno la Mungu ni kama kioo.'

Nia ya kioo ni kuonyesha mahali kuliko dhaifu ili uweze kurekebisha. Unapotazama kwenye kioo cha Mungu kamilifu, yaani Maandiko, kitakuonyesha amri ya dhambi na mauti katika maisha yak. Kwa hivyo, utafanya jambo kuhusu kile unachotazama kwenye kioo hicho.

Yakobo anakubaliana na nduguye Yesu wakati anapotueleza hapa kuwa ikiwa tutaitikia Neno la Mungu jinsi tunavyoitikia kioo, basi tutatambua kuwa Neno hilo liko hai. Hii ndio sababu tuna ushauri mkuu kutoka kwa Yakobo kuitikia Neno la Mungu vyema. Yakobo anafanya mzaha kuhusu mtu anayesoma Neno, lakini halitii kwa kusema kuwa ni sawa na mtu anayejitazama kwenye kioo kila asubuhi. Baada ya kuona uchafu ulio kwenye uso wake, huenda zake mara akisahau jinsi alivyo.

Wakati waumini wanapokosa kuwa watendaji wa Neno, wao huleta dini isiyo ya kweli. Dini ya kweli hutii Neno la Mungu kwa kuwatembelea wajane na mayatima na kwa njia ya kuishi maisha matakatifu.

Iana Mbili Za Imani

Katika sura ya pili ya waraka huu, Yakobo anaanza kwa kuandika kuhusu, ‘uso bandia’ na ‘uso wa kweli.’ Neno ‘mtu’ humaanisha ‘uso’ na linahusu hali yetu ya nje. Yakobo anaandika kuwa ikiwa tutawapima wale wengine kulingana na hali zao za nje, au ukosefu wa hali hizo, basi hilo ni dhambi, kwa sababu Mungu hupima watu kwa misingi ya kilicho ndani ya mioyo yao. Kulingana na Neno la Mungu, *‘….Bwana haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali Bwana huitazama moyo* ***(1 Samweli 16:7).’***

Kisha mwandishi huyu anazungumzia imani duni au bandia na ya kweli. Hili linatuongoza kwenye vifungu vyenye utata sana katika agano jipya ***(2: 14-26).*** Ingawa baadhi ya watu huona utata kati ya mkazo wa Paulo na Yakobo juu ya neema, kuna utata tu mmoja. Yesu alikubaliana na Yakobo aliposema, *‘Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua* ***(Mathayo 7:20).’*** Yesu pia anafunza kuwa mtu anayesikia mafunzo yake na kutotii, anajenga nyumba (uzima) bila msingi. Yakobo anakubaliana na nduguye anapoandika kuwa kazi ni matunda ambayo huzaa kwenye mti wa imani.

Mtu mmoja aliwahi kunukuliwa akisema hivi: ‘imani peke yake inaweza kuokoa, lakini imani ambayo hukoa sio peke yake.’ Tunaokolewa kwa imani peke yake, ingawa matendo yetu yanathibitisha kuwa imani yetu ni halisi, kwa sababu matendo huwa yanaandamana na kudhihirisha imani ya kweli.

SURA YA SITA
Aina Mbii Za Hekima

Kwenye sura ya tatu ya waraka huu wake, Yakobo anatazamia vyanzo vya sifa za kiroho ambazo hutuwezesha kuendelea katika imani. Anaandika kuwa mahali pazuri kuanzia kutekeleza sifa hizo za kiroho ni kujifunza kurudi ulimi wetu. Njia ile ya kufanya hivyo ni kuelewa kile tunachoita, ‘upole wa hekima.’

Nina uhakika unakumbuka kuwa hapo awali nilidokeza kuwa ‘Upole’ humaanisha ‘kuwa tulivu.’ Kabla ya farasi kutulizwa, huwa mnyama mwenye nguvu sana. Wakati farasi huyo anapotulizwa, bado huwa na nguvu zake lakini nguvu hizi

zinaweza kuelezewa kama ‘zilizoongozwa.’ Pia, maelezo, ‘upole wa hekima’ humaanisha, ‘upole ulioongozwa.’ Unapopokea hekima hii kutoka kwa Mungu, unapaswa kumwuliza Roho Mtakatifu akupe neema na adhabu ya kutekeleza hekima hiyo. Kwa maelezo mengine, unapaswa kuwasilisha maisha yako kwa Mungu ili aongoze, vile anavyofunua hekima yake kwako, jinsi farasi anavyowasilisha nguvu zake kwa lijamu na uongozi wa yule aliyepanda kwenye mgongo wake.

Maelezo hayo yanatufikisha kwenye mazungumzo ya hekima. Yakobo anatueleza juu ya aina mbili za hekima hapa duniani. Moja hutoka kwa Ibilisi ilhali ile nyingine kwa Mungu. Tunda ambazo hekima hizo zinazaa katika ‘bustani’ ya maisha yetu zinalingana na vyanzo vyake.

Kwa Muhtasari

Yakobo anataka tuelewe kuwa vyanzo vya nguvu ambazo zinaongoza maisha yetu. Ikiwa tunajaribiwa katika dhambi, na tunateseka kwa madhara yanayoambatana na dhambi hiyo, aina hiyo ya majaribu haitoko kwa Mungu. Unaweza kuletwa katika uhusiano pamoja na Mungu kupitia Neno Lake ambalo hukuwezesha kupanda juu ya nguvu ambazo zinanuia kukuvunja kiroho. Kupitia Neno hilo la Mungu, Yakobo anatushauri kushuhudia hekima ambalo hutoka kwa Mungu na kulipalilila katika bustani za maisha yetu.

SURA YA SABA
Vyanzo Vya Suluhisho

Yakobo amekuwa akitueleza kuhusu vyanzo na utaratibu wa dhambi na wokovu. Sasa anataka kutueleza kuhusu vyanzo vinavyohusika na utakaso- suluhisho mwafaka kwa shida za dhambi. Yakobo ana utakaso ndani ya moyo wake anapoandika sura ya tatu na ya nne ya waraka huu wake.

Sehemu hii ya waraka wake imejaa matumizi. Tambua mambo yale Yakobo anayotueleza tufanye. Nyenyekea kwa Mungu. Ikiwa unataka kufahamu msingi wa utakaso, ambao ndio suluhisho kwa hila za dhambi, basi nyenyekea kwa Mungu. Kunyenyekea kwa Mungu ni kitendo cha kiroho.

Kisha, sikiliza vile Yakobo anavyosimulia hila za ulinzi za kiroho wakati Ibilisi anapokujaribu kufanya dhambi. Dhahiri, Yakobo anasema, *‘…Mpingeni Shetani, naye atawakimbia* ***(Yakobo 4:7).’***

Wakati Yakobo anapotoa matumizi hayo ya mafunzo yake, tena anafanya sambamba mafuzo ya Yesu Kristo, ambaye ni ndugu yake. Yesu alifunza juu ya mfano mkuu wa mwana mpotevu, ambao uliwasilisha Mungu pamoja na upendo wake kama mzee anayekimbia kumkumbatia mwanawe anayerudi nyumbani baada ya kuishi nchi za mbali katika dhambi.

Wakati mwana mpotevu alipokuwa kwenye nchi za mbali, babeke alimruhusu ashuhudie madhara ya kutisha ya chaguo lake la dhambi. Hata hivyo, wakati mwana huyo anapochukua hatua ya kwanza kurudi kwa babake, mzee huyo anatoka huku akikimbia kumsalimia, na hilo ni picha ya upendo wa Mungu.

Hakuna jambo linaloshushia mzee heshima kama kuonekana akikimbia, ingawa hilo ndio picha Yesu aliyowasilisha katika upendo wa Mungu kwa mwanawe mpotevu

anayeamua kurudi kwa babake. Kwa hivyo, ushauri wa Yakobo, anapokubaliana na nduguye Yesu ni, *'mkaribie Mungu, naye atakukaribia.'* Yakobo anatufahamisha kuwa tunapochukua hatua ya kwanza kumkaribia Mungu, Mungu naye huja kwa kukimbia. Msingi, Yesu alifunza kuwa baadhi ya kweli ambapo anazungumzia kuhusu mfano wa mwana mpotevu.

Je, unaamini kuwa kweli Mungu anakupenda? Baadhi yetu tuna mtazamo mbaya kujihusu; tuna ungumu mwingi kuamini kuwa mtu ye yote anaweza kutupenda, hasa Mungu anayejua kila kitu kutuhusu. Tunapoongezea dhambi zetu mbaya katika mchanganyiko huo, huwa tunapata kuwa vingumu kuamini upendo ambao Mungu ako nao kwetu.

Niko hapa kukueleza kwa amri ya Neno la Mungu, kuwa Mungu ana kupenda! Upendo wa Mungu kwetu ni sawa na wa mzee anayekimbia kujithibitisha kwa mwanawe. Haijalishi unajihisi vipi, Mungu anakuenda tu!

Katika sura ya nne ya waraka huu, Yakobo anafafanua kwa busara nyingi ushari, matumizi na usawa wa Yesu. Ni sawa na maelezo ya kukimbia katika mafunzo ya Yesu.

Moja na mashauri mazuri sana ni mahali anapotukumbusha kuwa tuko mikononi mwa Mungu, majira yetu yako mikononi mwa Mungu; kila kitu kunachohisi kiko mikononi mwa Mungu. Tunapaswa kutambua kuwa ikiwa hatupatii neema, afya, na uzima, basi huenda hatutakuwa tukifanya cho chote mwaka ujao.

Katika sehemu inayobakia ya waraka huu, Yakobo anatupata 'utaratibu wa suluhisho za Mungu.' Yakobo anazungumzia swala la kuja kwa mara ya pili kwa Yesu Kristo. Sawa na mitume, anatueleza kuwa tukio hilo litakuwa suluhisho la mwisho kwa shida zinazotukumba hapa duniani. Kila mara manabii hao wa agano jipya au mwandishi wa agano hili wanapotufahamisha kuhusu mjio wa pili wa Yesu Kristo, matumizi huwa ya utendaji. Je, ni aina gani ya watu tunaopaswa kuwa sasa hivi, kwa hali ya kurudi kwa Kristo?

Hapo mwisho wa waraka huu, anaandika kifungu kizuri sana kuhusu, 'Uzima wa mwili wa Kanisa.' Hivi ndivyo tunavyotaja nyaraka hizi, ambapo tunamaanisha maisha ya mwili, Kanisa. Katika agano jipya, washiriki wote wa mwili wanashauriwa kuhudumu kwa washiriki na wale wengine wa mwili. Karama zote za kiroho zimefanywa kufundisha wema Kanisani.

Sura hili la mwisho pia linatupatia kifungu kikuu kuhusu uponyaji. Yakobo anatufundisha kuwa uponyaji unapaswa kufanyika wakati wale walio katika mwili wa Kristo wanapounganika pamoja. Haya yanahitaji kutajwa leo kwa sauti ya juu na wazi. Naamini katika uponyaji wa imani. Naamini kuwa Mungu huponya. Siamini kuwa ni mapenzi ya Mungu kila mara kuponya, bali naamini kuwa Mungu anaweza kuponya na kweli huponya. Uponyaji ambao Yakobo anasimulia hapa haufanyiki katika mazingira ya mkutano mkuu ulio na mponyaji wa imani akiongoza jambo hilo. Uponyaji huu hufanyika katika mazingira ya nyumba ya Kanisa.

Aliye mgonjwa anapaswa kuwa na imani kuu kuwaita wazee wa Kanisa lake. Kisha wazee hao wa Kanisa wanapaswa kuwa na imani kuu kuja wanapoitwa. Wakati wazee hao wanapokuja, wanashauriwa kuwekelea mikono yao kwa aliye mgonjwa na kummiminia mafuta. Kulingana na Yakobo, sio mafuta yanayomponya mgonjwa. Yakobo anasema hivi, '*kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa.'* (Pia ni jambo la ajabu kutambua kuw neno linalowakilisha mafuta sio yale mafuta ya kutibu. Kwa hivyo tunaweza kusema: chukua dawa yako kisha uombe).

Yakobo anazidi kutueleza kuwa ikiwa aliye mgonjwa ana dhambi, basi dhambi hizo zake zinapaswa kutubiwa, kisha aliye mgonjwa anapaswa kuhakikishiwa kuwa amesamehewa. Mara kwa mara hatia ya dhambi ambazo hazizatubiwa au kusamehewa inaweza kuwa sehemu ya maradhi.

Kuna kanuni nyingi sana za utendaji katika waraka huu mfupi wa Yakobo. Zisome, kisha umwulize Mungu azijumulishe katika maisha na Kanisa lako.

SURA YA NANE
Nyaraka ZA Petro-Petro Watatu

Katika agano jipya, tunakutana na Petro watatu. Kuna Petro tunayekutana naye katika vitabu vya Injili; Petro tunayekutana naye katika kitabu cha Matendo ya Mitume, kisha Petro huyu tunayekutana naye katika nyaraka hizi mbili. Katika Injili, Yesu alisema, *'Simoni, Simoni, tazama, Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano; lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike; nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako* ***(Luka 22: 31-34).'***

Hili ni sehemu ya ajabu sana kati ya mazungumzo ya Yesu na Petro kwa sababu neno 'kuongoka' na linazua maswali mawili: Kuongoka ni nini na ni lini Petro alipoongoka?

Kuongoka humaanisha: 'Kuwa na mgeuzo kabisa.' Kuongoka sio kuunganisha Kanisa au kubatizwa. Kuongoka ni ushuhuda wa kubadilishwa. Baada ya Petro kumkana Yesu, alitoka nje na kulia kwa majonzi. Alifahamu kuwa yeye hakuwa cho chote bila Yesu.

Baada ya kufufuka, Yesu akijitokeza kwa Petro. Huo ndio wakati Yesu alipomwuliza hivi, *'Je! Simoni wa Yohana, wewe wanipenda kuliko hawa?'* Saba kati ya mitume wote walikuwepo katika chumba cha orofani wakati Petro alipojigamba kuwa wenzake wanaweza kumkana Yesu lakini yeye hatawahi. Huu ni wakati Yesu alipomwuliza Petro hivi, *'Je! Petro wa Yohana, wewe wanipenda kulik hawa?'* Yesu alitumia neno la Kiyunani 'Agape' ambayo humaanisha aina ya upendo wa kujitolea kabisa, upendo wa ajabu.

Petro alijibu kwa ujasiri kwa kutumia neno la Kiyunani 'Phileo' ambayo ni sawa na kusema, *'Wewe wajua ya kwamba nakupenda kwa upendo uletao urafiki.'* Petro sasa hajigambi kwa sababu amevunjika moyo. Yesu alimwambia, *'Lisha wana- kondoo wangu!'* Kile Yesu anachosema hapa ni kuwa, *'Nakata mtu sawa na wewe anayejua maana ya kuanguka ili alishe kondoo wangu.'*

Kisha Bwana alimwuliza tena, *'Simoni wa Yohana, wanipenda? Sio zaidi ya maneno hayo bali ni unanipenda tu?* Kwa mara nyingine Yesu anatumia neno 'Agape.' *Naye Petro alijibu na kusema, 'ndiyo Bwana, wewe wajua kuwa nakupenda.' Bwana akamwambia, 'Chunga kondoo zangu.'*

Mara ya tatu Bwana alipotumia maneno hayo kumwuliza swali hilo, alisema, *'Simoni wa Yohana, wanipenda?' Kwa wakati huu Petro alihuzunika kwa vile alivyomwambia mara tatu, Wanipenda? Akamwambia, 'Bwana, wewe wajua yote; wewe umetambua ya kuwa nakupenda.' Yesu akamwambia, Lisha kondoo zangu.'* Wakati Yesu

alipojitokeza kwa Petro baada ya kufufuka na kumthibitishia kuwa ingawa alianguka, alikuwa bado amefunzu kuchunga na kulisha kondoo Wake, basi Petro alifahamu kuwa alikuwa mtu.

Katika kirabu cha Matendo ya Mitume, Petro na dunia yote walitambua kuwa Mungu anaweza tu kufanya kupitia mtu ambaye ametambua kuwa yeye si kitu. Kwa nini Roho Mtakatifu alimtumia Petro siku ya Pentekoste? Ni kwa sababu Petro alijua siri hizi nne za kiroho bora kuliko mtu ye yote:

> 'Sio mimi, ni Yeye, na niko ndani Yake Naye yuko ndani yangu.' 'Siwezi lakini Anaweza, na niko ndani Yake, Naye ndani yangu.' 'Sitaki kufanya, bali Yeye anataka kufanya, na niko ndani Yake, Naye yuko ndani yangu.' Sitaki, bali Anataka, kwa sababu nilikuwa ndani Yake, Naye ndani yangu.'

Tuna tofauti tatu za Petro katika Agano jipya. Uzima wa kiroho wa Petro katika Injili umejaa misukosuko, lakini Petro tunayekutana naye katika kitabu cha Matendo ya Mitume ni tofauti sana. Petro huyu ni thabiti sana. Baada ya Pentekoste, Petro haonekani kufifia.

Unaposoma nyaraka za Petro, unakutana na Petro wa tatu. Huyu ni mzee Petro. Petro alifahamu kuwa yeye si kitu na kuwa Mungu anaweza kufanya kupitia mtu ambaye si kitu kwa muda mrefu sana. Sasa ni mchungaji mzee anapoandika nyaraka hizi.

Anawaandikia wafuasi wa Kristo ambao walikuwa wa asili ya Wayahudi, waliokuwa wametawanyika kote katika *Asia Minor*, ambako nyakati hizi kunajulikana kama Uturuki. Walikuwa wametawanyika baada ya kudhulumiwa. Petro yuko mjini Rumi. Anapozungumzia Babeli, anamaanisha huko Rumi. Petro anajua kuwa mateso na dhuluma huko Rumi yanazidi kuwa mabaya na kuwa punde yataenea kote katika majimbo au mikoa ambako wafuasi wa Kristo wa asili ya Waebrania walikuwa wametawanyika. Nia yake kuu kuwaandika hayo, kama mchungaji, ilikuwa kuwafariji watu hao waliokuwa wanateseka. Hayo yanaonekana kuwa mkazo mkuu katika nyaraka zote mbili.

Kabla ya kusoma nyaraka hizi za Petro, ningependa kushirik nawe maono zaidi. Petro hangeweza kuandika wala kusoma. Hii ndio sababu anatuambia hapo mwisho wa nyaraka hizi kuwa, '*kwa mkono wa Silwano, ndugu mwaminifu kama nionavyo, nimekuwaandikia kwa machache****….(1Petro 5:12).'***

Unaposoma nyaraka hizi za Paulo, hautapata hoja zilizo na utaratibu. Tazama baadhi ya vipande vizuri sana, vya maana, vya injili na kiroho vya kweli ambavyo vinazungumzia kweli za kuinua Mungu na Yesu Kristo. Petro mara kwa mara anaruka kutoka hoja moja hadi nyingine huku akishiriki katika baadhi ya kweli ambazo ni vingumu sana kuelewa.

Kwa mfano: Petro anawasilisha mafunzo ya Yesu kwa roho huko gerezani. *Martin Luther* aliwahi kusema, 'Hakuna mtu ajuaye maana ya ujumbe huu.' Baada ya kuandika kifungu hiki kingumu, Petro punde anabadilisha hoja na kuzungumzia kuhusu Nuhu na gharika. Hoja hiyo inaleta lingine la ubatiso. Anashiriki nasi maono yake yenye uvuvio juu ya ubatiso. Kumbuka, Petro haandiki; bali anashikiri moyo wake.

Yohana ni mtume wa upendo. Paulo ni mtume wa imani. Lakini Petro ni mtume wa tumaini. Nyaraka za Petro zinwasilisha tumaini kwa watu waliokuwa wanateseka.

Petro tunayekutana naye katika Injili bila shaka alikuwa kafiri wakati alipokutana na Yesu. 'Thawabu' sio moja na maneno ambayo angetumia kwa wakati huu katika maisha yake. Neno 'thawabu' ni neno mzee angetumia. Petro tunayekutana naye katika

nyaraka hizi mbili ni mchungaji mzee ambaye kwake, Mungu ni wa thamani, Neno ni la thamani, wokovu ni wa thamani na watu wa Mungu ni wa thamani.

SURA YA TISA.
Waraka Wa Kwanza Wa Petro

Petro anawaandikia Wakristo Wayahudi ambao walikuwa wametawanyika kote huko *Asia Minor.* Huduma yake ilikuwa msingi kwa waumini Wayahudi. Petro anajaribu kuwatia moyo na kuwapa faraja katika mateso yao. Anawapa baadhi ya maono ya ajabu kwa nini Mungu hurusu watu wake kuteseka.

Anaandika akiwa mjini Rumi ambapo wafuasi wa Kristo wnadhulumiwa. Anajua kuwa dhuluma hizo zitazidi kuwa mbaya sana kisha kuenea kote katika majimbo ambako wapokezi wa waraka wake wanaishi. Kanisa katika kizazi chake cha kwanza lilishuhudia dhuluma kuu. Ama kwa kweli, kwa kipindi cha kwanza cha miaka mia tatu ya historia ya Kanisa, ilikuwa kinyume cha sheria kuwa mfuasi wa Yesu Kristo.

Petro anawasilisha mitazamo miwili kuu ya mateso kwa wale aliokuwa akiwaandikia. Moja yao ni ‘ikiwa kwa haja.’ Anaamini mara kwa mara Mungu huturuhusu kuteseka kwa sababu tunahitaji kuteseka. Maoni yake ya pili kuhusu kuteseka ni kuwa, baadhi ya mateso ni ya ‘majira.’ Kwa maelezo mengine, mateso mengi ni ya muda.

Anawasilisha maono yake ya tatu kuhusu kuteseka wakati anapolinganisha imani yao ya thamani na dhahabu. Dhahabu ni madini ya thamani sana na husafishwa kupitia moto. Vile Mungu anavyotazama katika maisha yao, mambo yaliyo muhimu kwake ni imani yao na kukua kiroho ***(1Petro 6-7).***

Wakati Petro anapotazamia swala hili la wokovu, anazungumzia dhana hili la kuzaliwa mara ya pili na uchanguzi. Manabii walikuwa wamebashiri wokovu uliohubiriwa siku ya Pentekoste. Anatoa maano ya ajabu sana, kuwa walipoandika, ingawaje waliandika kwa nguvu, uweza na uvuvio wa roho; hawakuelewa wakilichokuwa wakiandika. Anasema kuwa siku na wakati ambao wasomi wake wanaishi, wokovu huu umetimika, ambayo kwa uwazi yameandikwa katika fasihi ya unabii ya Neno la Mungu.

Tuna upunguvu mwingi wa mtazamo wa kihistoria ambao unakubali idadi ya watu waliokufa ili wengi wetu tuweze kuwa na baraka za kiroho tunazofurahia leo. Kwa mfano, tambua Maandiko, Neno lililoandikwa la Mungu. Tulipoanza mafunzo haya, nilishiriki nawe maono kadha kuhusu jinsi Biblia ilivyounganishwa. Mafunzo machache jinsi ya kuweka pamoja Biblia yatakusadia kutambua watu ambao wamewasilisha maisha yao kwetu ili waweze kupata Neno la Mungu jisni ilivyo siku ya leo.

Basi vile tunavyopata mtazamo huo wa kihistoria juu ya swala la wokovu, Petro anatukumbusha kuwa tunawiwa na deni kuu na watu wengi. Ikiwa ni wakati wa kuvuna, kumbuka kuwa watu wengi waliteseka wakati wa kupanda ili nawe uweze kuvuna mavuno hayo siku ya leo ***(Yohana 4:36-38).***

Petro anatukumbusha yale tayari tumejifunza tuliposoma vitabu vya Kutoka, Mambo ya Walawi, Kumbukumbu la Torati na Ruthu alipoandika kuwa Yesu alikuwa ‘Mkombzi wetu.’ Jinsi Boazi alivyomfanyia Ruthu, Yesu pia alitununua tena kwa Mungu

kupitia kifo chake, na kuturudisha kwa Mungu kupitia kufufuka kwake na kuleta uhusiano kati yetu (***1Petro 1:18, 19).***

Mawazo Ya Uzazi Wa Pili

Unapozaliwa mara ya pili, sio muhimu kuelewa ushuhuda huo kabla haujatendeka kwako. Hauhitaji kufahamu uzazi wako halisi wakati ulipozaliwa hapa duniani. Uzazi huo ulitendeka kwako. Kuzaliwa huko mara ya pili pia kunafanyika kwako kisha, unapotazama nyuma na kuwazia, basi unaelewa yale yaliyofanyika kwako.

Jambo la muhimu kuhusu ushuhuda wo wote wa kiroho sio maelezo, bali ni matokeo ya ushuhuda wenyewe. Hii ndio njia mtume huyu mashuhuri anavyoelezea kuzaliwa huku kwa mara ya pili: *'Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa Neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele* ***(1 Petro 22, 23).'***

Petro analinganisha kuzaliwa kwa kiroho na halisi. Anatueleza kuwa tunapozaliwa mara ya pili, mbegu, (neno la Kiyunani la shahawa) lilikuwa lisizoharibika. Petro anatueleza kuwa 'mbegu' lisiloharibika lilikuwa Neno la Mungu, na imani yetu limekuwa 'yai.' Tuliposikia Neno hilo la Mungu katika imani, Neno hilo limekuwa kama 'shahawa' lisiloharibika ambalo linazalisha 'yai' la imani yetu. Maisha ya kiroho yanafanyika ndani yetu tunapoliamini Neno la Mungu.

Petro pia anatupa maono kadha ya kiroho katika 'jinsi ya' kuzaliwa mara ya pili anapotueleza kuwa tunazaliwa mara ya pili tunapotakaswa roho zetu kwa kusikia, kuamini na kuitikia Neno la Mungu kwa utiifu.

Je, umewahi kushangaa uhusiano kati ya watu wa agano la kale na jipya? Hapa kuna kifungu ambacho kinawaleta makundi hayo ya watu pamoja. Katika agano la kale, Mungu alitaka kuwa na ufalme wake, lakini watu wa Israeli walimwendea Samweli na kumwambia kuwa hawakutaka Mungu awe mfalme wao.

Baada ya janga hilo la ufalme na utumwa na miaka mia nne ya kimya, Yohana pamoja na Yesu walikuja huku wakihubiri Habari Njema ya ufalme wa Mungu, ambao ulikuwa sawa na kusema, 'Mungu anataka kuwa mfalme wenu tena.' Yesu alielezea hivi, '*ninapozungumza kuhusu ufalme wa Mungu, umo kati yenu mnaonyenyekea kwa Mungu, kumtawaza mfalme katika maisha yao, na kuwa watumishi wake watiifu* ***(Luka 17:21, Yohana 3: 3-5).'***

Akiwaandikia wafuasi wa Kristo wa Kiebrania waliokuwa wametawanyika kote katika *Asia Minor,* Petro anawaeleza kuwa wao ndio tu taifa takatifu na kuwa ni watu wateule wa Mungu. .Pia anawaambia kuwa wao ni makuhani wa kiufalme (***1 Petro 2: 9, 10).*** Kuhani ni mtu anayekwenda mbele za Mungu na kuwatetea watu wale wengine. Watu hao pia walikuwa makuhani. Walikuwa wametumwa nje na Mungu kote duniani kufanya wanafunzi wa Yesu Kristo na kuwatetea kwa Mungu.

Pia anaandika, 'Ninyi ni watu wa taifa la Mungu' na 'mliokuwa kwanza si taifa.' Zaidi ya kuwa taifa takatifu, pia walikuwa makuhani wa kifalme, watu wa milki ya Mungu na waliokuwa si taifa hapo mwanzo.'

Kielelezo Cha Ndoa

Kwenye sura ya tatu ya waraka huu wa kwanza wa Petro, tunapata baadhi ya ushauri mwafaka wa ndoa katika Biblia. Wote wawili yaani Petro na Paulo wanasema,

‘*Wake, je, mnaona kielelezo cha Kristo na Kanisa? Katika kielelezo hicho, ninyi ni Kanisa. Waume, mnaona kielelezo hicho cha Kristo na Kanisa? Hicho ni kielelezo kilicho vuviwa cha ndoa na katika kielelezo hicho, ninyi ni Kristo.’*

Petro anaelezea ushauri huo ulio vuviwa wa ndoa kwa mke ambaye ana mume asiyetii Neno. Hayo yanaweza kumaanisha kuwa ameolewa na mtu asiyeamini wala hatii Neno la Mungu au angeweza kuwa anaamini lakini hatii kila mara Neno la Mungu.

Katika ushauri huo wa ndoa wa Petro na Paulo, mke anaambiwa kuwa mnyenyekevu kwa mume wake jnsi Kanisa ilivyo kwa Kristo. Sio jambo rahisi kuwa mnyenyekevu, lakini hilo sio shida kuu katika ndoa za watu wanaoamini. Shida kuu ni waume ambao hawafanyi kulingana na jukumu zao za kuwachunga wake na watoto jinsi Kristo alivyo kwa Kanisa.

Petro pia anatoa ushauri kwa mke kumvutia mumewe pasipo lile Neno. Petro anasema; Mumewe hatii Neno, kumaanisha kuwa hasimami mahali pake katika ndoa. Kabla ya kuandika aya moja kuhusu mume, Petro anamshauri mke wa aina hiyo kuwa wa kiroho, mtiifu, mnzuri na aliye nyamaza.

Tazamia neno ‘kutii’ vile tunapoendelea kuchunguza kielelezo cha ndoa Petro anachowasilisha. Hapo mwisho wa sura ya pili, Petro anaelezea kuhusu Yesu Kristo na kifo chake msalabani kama mtumishi anayeteseka ambaye alitabiriwa katika sura ya hamsini na tatu ya kitabu cha Isaya.

Maneno yake ya mwisho yanaelezea Yesu Kristo kama mchungaji na askofu wa nafsi zetu. Kisha anaelezea kielelzo hicho cha Yesu Kristo akichunga Kanisa, na kuanza ushauri wake kwa mke huyu kwa maneno haya, ‘kadhalika.’ Anamweleza mke huyu kuwa anapaswa kuwa mtiifu kwa mumewe, jinsi Kanisa ilivyo kwa Kristo.

NeNo ‘kutii’ katika hali ambayo Petro analitumia humaanisha ‘mwache mumewe akuchunge.’ Mungu amempa mume jukumu kuu. Mume anashauriwa na Mungu kushauri jinsi Kristo anavyochunga kanisa. Hiyo ni kumaanisha kuwa mume anapaswa kukupenda kwa upendo wa Kristo; anapaswa kukupa jinsi Kristo anavyopeana, anapaswa kuwa kwako jnsi Kristo alivyo kwa Kanisa. Paulo anatoa ushauri sawa na huo wa ndoa katika waraka wake kwa Waefeso (***5:22-25).***

Katika kikosi cha majeshi, kuna afisa mkuu. Huwezi kuwa na maafisa wawili wakuu. Anaweza kumpa mtu mwingine kazi. Hata hivyo, hawezi kupeana jukumu lake kuu. Ikiwa jambo litaenda mrama, yeye mwenywe ndiye atakayewajibika.

Katika ushauri wa ndoa wa Petro na Paulo, na kote katika Biblia, Mungu aliwapa waume jukumu la ndoa na jamii alipowaamuru kuwa wachungaji wa wake na watoto wao jinsi Kristo alivyo kwa Kanisa. Jukumu haimaanishi kuwa huwezi kuwa na maafisa wawili wakuu. Mtu mmoja sharti awe na jukumu kuu; naye Mungu hulitoa kwa waume.

Neno la kwanza ambalo Petro anaanza ushari wake kwa waume liko katika aya ya saba ni sawa na neno ambalo pia anaanza ushauri wake kwa wake. Tunaposoma neno ‘kadhalika’ tena, tunapaswa kujiuliza swali, ‘kadhalika ni nini Petro?’ Petro anatujibu na kusema: ‘rudini mtazame kielelezo cha ndoa. Je, unaona Kristo na Kanisa katika aya ya mwisho ya sura ya pili? Waume, katika kielelezo hicho cha Kristo. Kaeni na wake zenu kama Kristo kana kwamba mko pamoja na Kristo. Mwapende jinsi Kristo alivyopenda Kanisa. Jitoeni kwa wake zenu jinsi Kristo alivyojitoa kwa Kanisa. Kwa neema ya Mungu, simameni pahali penu kila mmoja. Jukumu Petro anazowapa wote wawili zinahitaji neema kutoka wa Mungu kutimiza. Changa moto kuu imepenwa kwa waume, kwa sababu wanapaswa kuwa jinsi Kristo alivyo kwa wake zao.

Vifungu Vingumu Vya Petro

Petro anamalizia waraka wake wa pili kwa maoni kuwa kuna mambo mengi yaliyoandikwa na Paulo ambayo ni vingumu sana kuyaelewa. Nafikiri kuwa Paulo tayari alikuwa amemwuliza Petro habari za vifungu hivi ambazo ningetaka kuzungumzia. Naanza kwa kutazamia kifungu kilicho kingumu kabisa katika nyaraka hizi za Petro, yaani ***(3: 17-4:2).***

Katika aya ya nane, Petro anaelezea juu ya hoja kumi. Anatueleza kuwa wakati Yesu Kristo alipokufa kwa ajili ya dhambi za dunia, ingawa mwili wake ulikufa, Roho wake alizidi kuishi, na ilikuwa katika Roho alipotembelea roho zingine huku gerezani na kuzihubiria-roho za wale waliokataa kusikiliza Injili walipokuwa na fursa hilo, jinsi ilivyokuwa nyakati za Nuhu.

Kadiri ilivyo, baada ya Kristo kufa msalabani na kupaa mbinguni, alikuwa na huduma katika ulimwengu wa roho. Kulingana na Petro, Kristo alikuwa na huduma ya ukombozi katika ulimwengu wa roho. Kwa kunukuu maneno ya Petr, kifungu hiki kinasimulia mambo ambayo, 'malaika walio na hamu yanayotazamia', kwa hivyo ni vingumu sana kusema kwa ujasiri.

Petro anasema kuwa kuwa mwisho wa mambo hayo yote unakaribia na kuwa hali hiyo, ndio watu watakatifu wanaopaswa kuwa. Hapa, Petro anatupa baadhi ya maono ya ajabu katika karama za kiroho na huduma ambazo zimewezeshwa na karama hizo.

Kulingana na jitu hili la kiroho la utendaji, haijalishi karama yako ni lipi, hivyo ndivyo mtazamo wako wa huduma unavyopaswa kuwa. Ikiwa karama yako ni kuhubiri, basi hubiri. Mtindo unaofahamika sana ni kuwa uthibitishe subira yako kwa kuwa tayari kufanya cho chote. Kila mtu hufanya kila kitu. Mafunzo yote katika Maandiko kuhusu karama za kiroho yanatukumbusha kuwa ni ya aina mbalimbali na kuwa yametolewa kwa kila mtu anayeamini jinsi Mungu apendavyo. Zinatolewa na Roho Mtakatifu kumdumisha Kristo, na kutia moyo mwili wa Kristo. Kupitia karama zako za kiroho, unanihudumia ilhali kupitia karama zangu za kiroho nami nakuhudumia.

Jinsi Petro anavyoendela kusema katika sura ya nne, anatupa ushauri zaidi kuhusu kuteseka. Ikiwa unateseka, Petro anasema, '*Msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho **(1Petro 4:12).'*** Tunafikiri kuwa shida na misiba au mateso ni wavamizi, janga, na maafa ambayo hayapaswi kufanyika. Hatuwezi kuelewa kuwa ni nini inayotendeka kwetu. Katika sehemu nyingi duniani, watu wamekuwa wenye uhakika. Wanajua kuwa misiba ni sehemu ya maisha. Jambo moja ambalo linatofaitisha mtu mmoja na mwingine sio ikiwa au la ana msiba, bali ni jinsi anavyokabilina na msiba au mateso yake.

Unawajibika kwako mwenyewe. Huenda hauwajibiki kwa kila jambo linalotendeka kwako, lakini unawajibika kwa yale utakayofanya kuhusu mambo hayo. Hoja ni vipi utakavyoitikia misiba hiyo yako?

Sote tuna mawimbi lakini pia tuna neema na nguvu za Mungu kutuwezesha. Mungu ametupa Neno Lake, ambalo ni kifaa chetu cha kuamini. Tunapopitisha mawimbi yetu kwenye kifaa hicho, kupitia Neno, Mungu anaweza kutupa hekima ya kukabiliana na shida zetu. Pia anaweza kutupa neema ya kutumia hekima hiyo. Jamabo hilo linaleta kile Petro anachotaja kama 'shahidi.' Mungu huruhusu mawimbi kwa sababu anataka tuwe mashahidi wake. Tunaweza kuwa mashahidi wema, au wabaya, lakini ukweli ni kuwa, tu mashahidi.

Kwa mfuasi mwaminifu wa Kristo, misiba au mateso ni mwito. Umeokolewa kwa sababu Mtu fulani aliteseka. Umeitwa kufuata hatua Zake. Umahesabiwa pamoja naye-mshiriki wa mateso Yake. Baadhi ya watu husema kuwa Mungu hataki watu wake wateseke. Lakaini hapa, Petro anaelezea wazi kuwa mara kwa mara, wao wateswao kwa mapenzi ya Mungu na wamwekee amana roho zao, katika kutenda mema, kama kwa Muumba mwaminifu (***1 Petro 4:19).'***

Neno kwa Wazee

Sura ya tano imeelezewa kwa wazee wa Kanisa. '*Mimi niliye mzee, mwenzi wao.*' Petro ni mzee pamoja na hao wengine. Jinsi tulivyotazama kwenye sura ya tatu ya utangulizi wetu kwa maandishi ya Petro, tunaelewa kwa nini. Anawaeleza kuwa wanapaswa kuchukua jukumu la kuchunga la Kanisa, sio kama mabwana, bali kama mifano.

Unaposoma utaratibu wa uongozi wa Kanisa, haupataka cho chote hapa duniani cha kulinganisha na Kanisa la kama shirika. Kanisa halipaswi kuwa kama kampuni ambalo linaongozwa na Rais, anayemiliki mali pamoja na wafanyi kazi. Jambo lile mzee wa Kanisa analopaswa kufanya ni kuwa mfano wake. Ikiwa mfano wake unavutia watu, basi nao watakuja kwake tafuata ushauri. Hilo ndilo kazi wachungaji wanalopaswa kuwa nalo katika Kanisa, bali sio amri jinsi ilivyo katika kikosi cha majeshi au kwenye biashara.

Mtu aliyemfunza Petro aliwahi kunena haya: *'hupenda kusalimiwa masokoni, na kuitwa na watu, Rabi. Bali ninyi msiitwe Rabi, maana mwalimu wenu ni mmoja, nanyi nyote ni ndugu. Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni. Wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo. Naye aliye mkubwa wenu atakuwa mtumishi wenu. Na ye yote atakayejikweza, atadhiliwa; na ye yote atakayejidhili, atakwezwa (**Mathayo 23:7-12.***

Petro anatamatisha waraka wake wa kwanza kwa maelezo ya historia ya maisha yake. Anaandika: *'na Mungu wa neema yote, aliyewaita kuingia katika utukufu wake wa milele katika Kristo, mkiisha kuteswa kwa muda kidogo, yeye mwenyewe atawatengeneza, na kuwathibitisha, na kuwatia nguvu **(1 Petro 5:10).'*** Baada ya Petro kuteseka kwa muda, Mungu alimfanya kuwa mkamilifu na imara. Mungu alimtengeneza, kumthibitisha na kumtia nguvu. Na ni Petro huyu wa tatu aliyeandika maneno haya. Aya hiyo moja ndio hadithi ya maisha ya Petro. Petro anasema, 'hapa kuna kusudi la baadhi ya mateso:

Mungu ni mwenye haki akijaribu kuwaimarisha, na kwa hivyo, janga, maafa ambayo yanawakumba yanamaanisha kuwa kuwa muda, Mungu anarudi na kukuchukua kisha kukufanya thabiti na kukuimarisha milele kwa sababu umekuwa katika ushuhuda wa kuteseka.'

SURA YA KUMI
Waraka Wa Pili Wa Petro

Petro alifahamu kuwa alikuwa afe wakati alipoandika waraka wake wa pili. Punde tu alipowasilisha wosia wake wa mwisho na agano katika waraka huu wake kwa

Timotheo, anashiriki nasi maneno yake ya mwisho kwa kondoo alioahidi Bwana kuwa atachunga katika waraka wake wa pili.

'Kurudia ni msingi wa elimu.' Mchungaji mmoja mwalimu aliwahi kunulikuwa akisema hivyo. Akijua kuwa siku zake zilikuwa chacxe, mchungaji huyu mzee anakuja mikono na kushiriki moyo wake katika baadhi ya mambo ambayo anajua kuwa wasomi wake tayari wanajua ambayo anataka wakumbuke.

Petro anatueleza katika aya za utangulizi kuwa neema na amani zinaweza kuongezewa kwetu kupitia ufahamu wa Mungu na Yesu Kristo Bwana wetu. Katika aya ya tatu ya ujumbe wake wa kwanza, anakumbusha kondoo wake kuhusu jambo ambayo labda aliwaambia mara nyingi: *'Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa.'* Kisha Petro anawaleza wasomi wake jinsi wanavyoweza kuzipata kwa kusema, *'kwa kumjua Yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe.'* Jambo hili linamwongoza kwa ujumbe huu: *'Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu.'*

Mambo haya yanayohusu maisha na tabia ya Uungu yanakuja kwetu kutokana na uhusiano wetu pamoja na Mungu na Kristo. Kulingana na Petro, hizo ni ahadi za thamani na kwa utekelezaji wake, tunaweza kuwa washirika kwa tabia za Uungu.

Tunaamini leo kuwa maarifa ni sifa. Hata hivyo, katika mambo ya kiroho, Maandiko yanatufahamisha yale tuliyoyasikia kutoka kwa manabii, kutoka kwa Yesu, na tunasikia sasa kutoka kwa mtume Petro- kuwa maarifa sio sifa. Matumizi ya maarifa ndio sifa. Tambua kuwa Petro haandiki kuwa, *'katika maarifa yenu tieni imani.'* Bali anaandika kuwa, *'katika imani yenu tieni maarifa.'*

Sifa ni matumizi ya imani yako ambayo inaleta wema. Sifa ni mhusika. Unapofaulu katika sifa, au kuhusika wa Kikristo, basi tia maarifa. Jambo la muhimu ni kuwa, 'kifungu hiki kinasema nini? Kinamaanisha nini? Kinamaanisha nini kwako? Na unakijumulisha vipi katika maeneo ya utendaji ya maisha yako?' Ni katika matumizi ya Maandiko yanapokuwa nguvu za kiroho ambazo yanapaswa kuwa. Kulingana na Petro, tunapaswa kupitia katika sifa yetu ya imani, kisha la maarifa.

Petro anazidi kusema, *'na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo.'* Maongezi haya yanawakilisha moja ya vifungu vizuri sana katika Maandiko kuhusu swala la kuimarika kiroho. Kisha, ikiwa wanafunzi wanashuhudia maongezi hayo ya imani, basi tunao ahadi tatu: 'ukiongeza mambo hayo katika imani yako, kwa neema ya Mungu, utakua kiroho, na utakuwa na uzao mwingi. Utaweza kuishi imara na vema kwa Bwana na kuthibitisha kuwa u mmoja wa walioitwa wa Mungu. Utafanya mwito wako na uteuzi kuwa wa hakika. Utaingia mbinguni, na hadi uingie, hautawahi kuwa imara au thabiti.

Petro anaanza maneno yake ya mwisho ya hekima kwa neno ya ushuhuda wa kibinafsi: *'kwenye mlima wa mageuzi kisha nalimwona Bwana Yesu Kristo akigeuzwa.'* Petro anasema, '*ingawaje nimekuwa na ushuhuda kamilifu ningependa kuwaarifu jambo. Neno la Mungu ambalo limekuja kwetu kupitia utaratibu huu wa uvuvio ni la hakika kuliko ushuhuda wangu kwenye mlima wa Mageuzo.'*

Petro anatufahamisha kuwa tunapaswa kutenda vema kuja kwa Neno hilo la Mungu kana kwamba tunakuja kwa taa ing'aayo mahali penye giza. Tunapokaribia nuru hilo, jambo fulani linatendeka katika mioyo yetu. Petro analisimua vema: '*Mpaka*

kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwetu.' Je, nyota hii ya asubuhi ambayo inang'aa mioyoni mwetu ni gani? Nyota hilo ni Yesu aliyefufuka aishiye. Petro anatueleza jinsi Kristo anavyozaliwa ndani yetu.

Ni jambo la ajabu kuwa Petro na Paulo wote wanatupa jumbe kuu kuhusu Neno la Mungu katika Maandiko yao ya mwisho kwa Kanisa na dunia. Petro anafanya hivi kwenye sura ya kwanza ya waraka wake wa pili kwa Timotheo. Paulo anatueleza Neno la Mungu lina uvuvio, ilgali Petro anatueleza maana ya uvuvio huo. Petro anatueleza kuwa wale walioandika Maandiko hayo yaliyo na uvuvio waliongozwa na Roho Mtakatifu jinsi upepo unavyovuma na kusukuma chombo kwenye bahari. Petro analinganisha ujumbe wake kuhusu uvuvio na Maandiko na ushuhuda wa kizazi kipya.

Sura ya pili iko sawa na waraka wa Yuda, kwa hivyo hatutapoteza muda mwingi katika kuchambua. Sawa na Yuda, waraka wa pili wa Petro sura ya pili ni laana kwa walimu wa uongo. Kwenye sura ya tatu, Petro anaandika kuhusu, 'Siku ya Bwana.'

'Siku ya Bwana' ni moja ya matukio kati ya mfululizo wa matukio yanayojulikana kama 'kuja kwa mara ya pili kwa Yesu Kristo.' Mjio huu wa pili wa Yesu Kristo sio tukio moja; bali ni mfululizo wa matukio, pamoja na kunyakuliwa kwa Kanisa, Dhiki Kuu, ufalme wa Mungu hapa duniani na ufufuo au kiyama. Lakini mwisho kati ya matukio haya ambayo yanajulikana kama 'mjio wa pili wa Yesu Kristo' ni 'Siku ya Bwana.'

'Siku ya Bwana' ni tukio lililohubiriwa na manabii wengi na linahusu kufumuliwa kabisa kwa kila kitu hapa duniani. Yesu alisema, *'mbingu na nchi zitapita.'* Petro naye anaelezea wazi kuwa ardhi na mbingu zitaangamizwa. Zitafumuliwa kwa moto mkali.

Tangu tukio la Hiroshima na Nagasaki, tunafahamu kuwa binadamu anaweza kufanya vile Petro na manabii wale wengine walivyobashiri. Mungu alifanya hivyo mara moja kwa njia ya maji na sasa anayaweka kusubiri moto mkuu. Kulingana na Petro, jambo hilo litatukia sawa na jinsi manabii walivyosema.

Hatufai kufikiri kuwa anajikokota katika kutimiza hayo kwa sababu siku na majira yako mikononi mwa Mungu. Kwa hivyo, kwa nini husubiri? Sababu ile tu Kristo hajakuja na kuazisha mfululizo huu wa matukio ambayo hatimaye yataleta 'Siku ya Bwana' ni kuwa, Mungu anataka kuwasilisha Injili kwa watu wa dunia waliopotea. Hanuii kuwapa wachache fursa ya wokovu.

Petro anasema kuwa tunaweza kuharakisha siku hii sawa na vile tunavyoshuhudia Kristo na kuwasilisha Injili kwa watu ambao bado hawajawahi kulipata. Swali ile tunalopaswa kuuliza vile tunavyotazama maelezo haya ya kutisha ya mjio wa pili wa Yesu Kristo ni: 'Je, ni watu wa aina gani tunaopaswa kuwa kwani tunaona kuwa vitu hivi vyote vitaangamizwa?

SURA YA KUMI NA MOJA
Waraka Wa Kwanza Wa Yohana.

Nataja aya za mwanzo kumi na suita za waraka huu wa kwanza wa Yohana kama 'dira ya hakikisho.' Hakikisho ni mada ya waraka huu wote. Je, unao uhakika kabisa kuwa dhambi zako zimesamehewa na kuwa ikiwa utakufa sasa hivi, utakwenda mbinguni? Ukiwa unakosa hakikisho hilo, basi unapaswa kusoma waraka huu.

Mwandishi, ambaye pia ndiye aliyeandika kitabu cha Ufunuo wa Yohana, na nyaraka zingine mbili fupi ambazo zimepewa jina lake, anatueleza kusidi lake la kuandika. Aliandika Injili ya Yohana ili tuweze kuamini na kuwa na uzima wa milele. Anaandika waraka huu kwa wale ambao tayari wameamini, ili waweze kujua, kuwa hakika wanaamini. Kwa maelezo mengine, anaandikia wale ambao wanatazamia hakikisho, yaani hakikisho la wokovu wao. Ikiwa hauko imara kiroho, na hauna hakikisho kamili la wokovu wako, Yohana anasema, '*Nimewaandikia ninyi mambo hayo* ***(Yohana 20:30, 31, 1 Yohana 5: 13).'***

'Ikiwa tunajua kuwa mtu hajui, na hajui kuwa kweli hajui, basi yeye ni mjinga. Mwambae. Ikiwa mtu hajui, na anajua kuwa hajui, ni mwana. Mfunze. Na ikiwa mtu anajua, na hajui kuwa anajua, basi amelala. Mwamshe. Lakini ikiwa mtu anajua, na anajua kweli kuwa anajua, basi naye ni kiongozi. Fuata yeye.' Yohana anaandika waraka huu kwa watu wanaofahamu kuwa wanaweza kuwa wanajua kuwa wanajua kwamba wanao wokovu.

Aya za mwanzo kumi na sita za waraka huu wa kwanza wa Yohana zinawasilishwa kwetu, sawa na vile Injili ya Yohana inavyofanya, aina ya mtazamo wa yale Yohana atakayotueleza. Sote tunahitaji dira ya kiroho. Tutalipata 'Dira la Hakikisho' kwenye waraka wa hakikisho. Sawa na vile kuna sehemu nane kwenye dira, hapa kuna hoja nane ambazo tutazipata kwenye dira hili la hakikisho la mtume Yohana: Hoja ya kwanza ni <u>kweli au hakika.</u>

Yohana anatueleza kuwa imani inahusu hakika au kweli. Imani sio hatua kwenye giza au kwenye nuru. Jinsi tulivyojifunza kwenye sura ya imani ya Biblia, imani inahusu thibitisho. Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo. Hilo ndilo tofauti kati ya mambo yatarajiwayo na imani. Bila thibitisho ambalo linakupa msingi wa mambo hayo yatarajiwayo, yale tunayoweza tu kufanya ni kutarajia. Lakini imani limekuwa kila mara na msingi wa hakika ambalo limejengwa juu.

Yohana anaandika kuhusu Kristo aliyefufuka wakati anapoanza waraka huu kwa kutueleza kuwa, *'Lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia, tuliloliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa, kwa habari ya Neno la uzima. Imani yetu kwa Krito aliyefufuka linatokana na hakika.'*

Unapolinganisha vitabu kama Injili ya Yohana na vitabu vingine vya agano jipya, kuna hakika mbili za Injili zinazojitokeza: Kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo. Paulo aliwaandikia Wakorintho kuwa: *'….Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo Maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo Maandiko. Hayo ndio niliyowahubiri huko Korintho. Hayo ndiyo mliyoamini na mnayoamini ambayo yalimwokoa* ***(1Wakorintho 15:1-4).'***

Hoja ile nyingine kwenye 'dira ya hakikisho' ni <u>imani.</u> Unapaswa kuweka imani yako katika hakika hizo mbili. Hoja ya pili ni imani katika hakika. Nayo hoja ya tatu ni matokeo ya kuweka imani katika hakika ya kifo cha Yesu Kristo, ambalo linafanya tofauti zote hapa duniani! Dhambi zako zimesamehewa!

Kile Yohana anachotujenga hapa katika Dira hili la Hakikisho ni: Ikiwa kweli una imani katika hakika ya kifo cha Yesu Kristo msalabani, basi unao <u>msamaha.</u> Matokeo ya kuweka imani katika hakika ya kifo cha Yesu Kristo ni msamaha. Namaanisha msamaha kabisa.

Hoja ile nyingine kwenye dira hili ni matokeo ya kuamini katika kufufuka kwa Yesu Kristo- unaweza kuja na kuwa na ushirika pamoja na Kristo aishiye.

Neno ushirika humaanisha sawa na uhusiano au kuwa na umoja. Sawa na jinsi Yesu alivyoingia kwenye chombo kidogo cha Petro na kukijaza kwa samaki, pia anaweza kuingia katika chombo chako- maisha yako- na kuwa pamoja nawe. Anamaanisha kuwa cho chote alicho nacho kwa hali ya mali ni chako. Ikiwa uko katika ushirika pamoja naye, basi cho chote ulicho nacho ni chake. Ushirika ndio hoja ya nne katika 'Dira hili la Hakikisho.'

Hoja ya tano kwenye dira hili ni kufuata Kristo. Wakati watu walipomwambia Yesu kuwa wanamwamini, Alikuwa akiwaambia, 'Nifutaeni.' Yohana atataja tena na tena kuwa, '*Yeye asemaye ya kuwa anaakaa ndani Yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama Yeye alivyoenenda* ***(2:6).***' Hivi ndivyo tunavyofahamu kuwa tuna imani halisi na uzima wa milele.

Baada ya kufuata, hoja inayofuatia kwenye dira hili ni uhuru. Kwa maelezo, Yesu alisema kwenye sura ya nane ya Injili ya Yohana kuwa, *'Ninyi mkikaa katika Neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli..'* Kufuata au kuwa mwanafunzi kunahalalisha na kukuza imani. Lakini pia anaelezea matokeo ya kumfuata. Anasema kuwa, '*Tena mkifahamu kweli, (hakusema kwa muda gani), mtajua ukweli (na alitumia neno linalomaanisha 'kujua kwa uhusiano'), na hiyo kweli itawaweka huru* ***(Yohana 8:30-35).'***

Yohana anasema, '*nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali kwa dhambi za ulimwengu wote* ***(1 Yohana 2:1, 2).***' Unaona, inawezekana kuwa huru kutokana na dhambi.

Hoja nyingine ya Dira la Hakikisho ni 'utimizo.' Kwenye *1:4,* Yohana anasema, *'na haya twayaandika, ili furaha yetu itimizwe.'* Yale tuliyo nayo ni ya hakika na ya kweli, lakini kuna mengi. Yohana anataka tuwe na ushuhuda wa kutimiziwa. Tunaweza kuutaja kama 'utimizo.'

Nayo hoja ya nane ni uzao. Yesu aliwaambia mitume jinsi wanavyoweza kuwa na uzao kwa sababu alitaka furaha yao itimizwe. (***Yohana 15:11)*** Yohana anaamini kuwa baadhi ya tunda la Mungu katika ushuhuda wa Kristo yataleta hakikisho katika safari yetu ya imani.

Tunakuja katika ushuhuda wa kiroho jinsi tunavyokuwa kwa jambo lo lote lingine, tukiwa na nia moja ya fikira. Je, ni nini iko ndani yangu? Lakini vile tulivyoona katika kubadilishwa kwa Sauli wa Tarso, kweli tunaweza kuimarika tunapouliza swali hili: 'Bwana, unakata nikufanyie nini?' Vile Bwana anapojibu swali hilo kwetu, Biblia inataja jibu hilo kama 'kuwa na uzao.'

Kwa muhtasari, hoja hizi nane kwenye Dira ya Hakikisho ni: Hakika, imani, msamaha, ushirika, kufuata, uhuru, utimizo na uzao. Ukipata kuwa hauna uzao, ua kuwa hauna timizo, basi rudi kwa dira tena.

SURA YA KUMI NA MBILI
Upako Unaohakikisha.

Katika sura ya pili, Yohana anaendelea kutueleza jinsi tunavyoweza kujua kuwa tunaamini na kuwa na uzima wa milele. Anatufahamisha kuwa tunaweza kujua kuwa tunaamini tunapopenda ndugu zetu. Yohana anaandika, *'Ampendaye ndugu, yuko ndani*

ya Kristo. Mtu huyu kweli ni muumini wa kweli. Na asiyependa ndugu, yumo gizani hata sasa.'

Kisha anatufahamisha kuwa tunajua kuwa tunao imani halisi na uzima wa milele tunapopenda Baba zaidi ya jinsi tupendavyo dunia. Mambo ya dunia ndio wazo lililokuwa ndani ya akili ya Yohana. Dunia ina dhamba ambayo inazunguka kwenye mambo ya thamani za kidunia, hali ya maisha na jinsi ya kufikiria. Yohana anatueleza hapa kuwa tunaishi na kulipenda dunia hii, kisha hatumpendi Mungu.

Vile anapoendelea, anatupatia njia nyingine ambazo tunaweza kuthibitisha hakika letu. 'Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua Yeye, kwa sababu Roho Mtakatifu anaweka kanuni safi.' Kuna hali ambapo Yohana kweli anasema hapo kuwa, 'unajua hayo kwa sababu unajua kwa sababu unajua.'

Yohana anatueleza kwenye aya ya ishirini kuwa, '*nanyi mmepakwa mafuta na Yeye aliye Mtakatifu nanyi mnayajua yote.'* Kisha kwenye aya ya ishirini na saba anaandika, '*nanyi, mafuta yale mliyoyapata kwake yanakaa ndani yenu, wala hamna haja ya mtu kuwafundisha..'* Kufafanua aya hili, Yohana anasema, 'mafuta haya yanaweza kuwafunza.' Na wakati mafuta haya yanapowafunza mambo ya kiroho, unakuwa na thibitisho lingine ndani yako. Ikiwa Roho Mtakatifu anaishi ndani yako na anakufunza, basi umetambua msingi mwingine wa hakikisho la imani yako na uzima wa milele.

Moja ya kazi za huyu anayekaa ndani yenu ni kukufunza kweli za kiroho. Inaonekana kuwa misingi ya kanuni hizi za ushirika katika Kanisa la agano jipya ni muhimu sana. Paulo aliandika: '*hakuna mtu asemaye kuwa Yesu ni Bwana ila kwa Roho Mtakatifu.'* Yohana anatueleza kuwa hili ni jaribio la kanuni ambazo kupitia kwake, unapaswa kuwataini watu: Je, unaamini kuwa Yesu ni Kristo? Hilo ni swali mwafaka kuuliza unapohitaji kutambua mahali wako kiinjili.

Kuna majibu tofauti ya watu ambao walijibu wakati swali hilo lilipoulizwa kwa kusema: 'Hakuwa Kristo. Alikuwa na viungo vya Kikristo ndani yake, sawa na ilivyo kwa Budha na Gadhi. Watu wengi wamekuwa na viungo hivyo vya Kristo ndani yao, lakini Yesu si Kristo.' Yohana anaandika kuwa ikiwa tunakana kuwa Yesu ni Kristo, basi tu wapinga Kristo na waongo kwa sababu Yesu ni Kristo (***1 Yohana 2: 22).***

Kwenye sura ya tatu, Yohana anatueleza kuwa tuna aina mbili za watu hapa duniani. Tuna wana wa Mungu wa wa Ibilisi. Yohana anatufahamisha kuwa ikiwa unataka kutambua tofauti, ni jambo rahisi. Anaelezea hivi katika sura ya tatu: *'atendaye dhambi ni wa Ibilisi.'* Wao huwa kila mara wakitenda dhambi. Ni tabia yao kutenda dhambi. Lakini wana wa Mungu hawatendi dhambi. Mtindo wao sio wa kila mara.

Jinsi nilivyoelezea kwneye sura ya kwanza, kwa lugha ya Kiyunani, ngeli iliyopo inawakilisha wakati unaoendelea. Yohana hasemi kuwa wana wa Mungu hawawezi kutenda dhambi, au hawatahi kutenda dhambi. Bali, anamaanisha kuwa wanapotenda dhambi, huwa wanaanguka ndani yake. Dhambi sio jambo asili kwao. Wana wa Ibilisi huwa na tabia kila mara ya kutenda dhambi, ilhali wana wa Mungu ni kinyume. Tunaposhuhuda mtindo huu kwenye maisha yetu, tunajua kuwa tunaamini na tunao uzima wa milele.

Hapo mwisho wa sura ya tatu, Yohana anaandika tena kifungu kingine kikuu cha hakikisho. Tunapogumbikwa na dhiki, au jinsi Yohana anavyosema hapa, *'wakati moyo wako unapokuhukumu,'*unapotea kwa sababu ya hisia zako? Na wakati moyo wako usipokuhukumu, unakuwa na hakikisho la uzima wa milele? La! Wakati moyo wako unapokuhukumu, kumbuka kuwa: Mungu ni mkuu kuliko moyo wako. Mungu ni

mkubwa kuliko jinsi unavyojihisi. Wokovu wako hautokani na kitu kama hisia zako. Bali wokovu unatokana na ukweli kamili kuwa unaamini- na kuwa unamtii Bwana ***(3:19-22).***

SURA YA KUMI NA TATU
Kukiri Kunaothibitisha.

Kwenye aya za utangulizi katika sura ya nne, Yohana anatueleza jinsi ya kujaribu roho. Anatuonya kuwa roho wengi wa uongo wako hapa duniani, kisha anatuonyesha jinsi ya kutambua tofauti kati ya roho wabaya na wema: '*Kila roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu. Na kila roho isiyomkiri Yesu haitokani na Mungu. Na hii ndiyo roho ya kumpinga Kristo ambayo mmesikia kwamba yaja; na sasa imekwisha kuwako duniani.'*

Je, roho inakiri vipi kuwa Yesu amekuja katika mwili? Mtume wa upendo anajibu swali hilo. Tunapopendana huwa tunakiri kuwa Yesu Kristo amekuja katika mwili. Kwa njia hii, Yohana anatueleza kuwa tunaposhuhudia Roho wa Kristo anayetenda ndani na kupitia mwili wetu, basi huwa tumepata njia ambayo tunaweza kuwa na imani na uzima wa milele. Anakubaliana na mtume Paulo kuwa tunda la Roho ni upendo ***(Wagalatia 5: 22, 23).***

Kisha anawasilisha sababu kumi kwa nini tunapaswa kupendana ***(4:7-12).*** Kwanza kabisa, tunapaswa kupedana kwa kuwa <u>pendo latoka kwa Mungu.</u> Ni wale tu walio na roho ambao wanakiri upendo wa Kristo wanaoweza kupendana kwani upendo wa kweli hutoka kwa Mungu.

Tunapaswa kupendana kwa sababu vivi ndivyo unavyoweza kutambua wanafunzi halisi wa Kristo kati ya wale ambao wanadai kuwa wanafunzi: Kila apendaye <u>amezaliwa na Mungu</u>. Wale ambao hawapendi hawajazaliwa na Mungu. Jambo hilo linafanya roho kuwa wa kawaida sana.

Sababu ya tatu ya Yohana inapatikana kwenye aya ya nane ya sura ya nne. Tunapaswa kupendana kwa sababu <u>Mungu ni pendo</u>. Upendo ndio maana ya Mungu. Upendo ni nafsi ya Mungu. Ikiwa unasema kuwa umezaliwa na Mungu, basi vitambulisho vyako vinapaswa kuwa upendo.

Kwenye aya ya kumi na ya kumi na moja, Yohana anasema kuwa tunapaswa kupendana kwani tumepewa mfano mkuu wa upendo. Yohana anaelezea juu ya Yesu Kristo akifa msalabani na kusema, *'wapenzi, na ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana.'* Kwa hivyo, inaonyesha kuwa tumekubaliana na Injili unapopendana kwa upendo wa ajabu.

Kwenye aya ya kumi na sita, Yohana anaandika: *'…Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake.'* Fikiria kuhusu Mungu akiwa kando yako, kama Mungu aliye na pendo anayekata kuwapenda watu wanaokutesa. Upendo ni vile Mungu yuko. Mungu ni pendo. Kwa hivyo, ikiwa utaishi ndani ya upendo huu ambao ni Mungu, <u>utaishi ndani yake, naye ataishi ndani yako</u>. Wakati jambo hilo linapotendeka, naamini utakapa njia nyingine ambalo unaweza kuamini na kuwa na uzima wa milele.

Yohana anasema kwenye aya ya kumi na saba ya sura ya nne kuwa ni sharti tupendane kwani ikiwa tutafanya hivyo<u>, tutakuwa na ujasiri katika siku ya hukumu,</u> katika hali ya umilele. Unapofikiri kuhusu hayo je, huwa unafikiri kuwa utakaribia kiti

hiki cha hukumu kwa ujasiri? Yohana anatueleza kuwa ikiwa tutapendana jinsi tunavyopaswa, basi tunapaswa kukaribia kiti cha hukumu kwa ujasiri.

Yohana anaandika kwenye aya ya kumi na saba, kuwa tunapaswa kupendana kwani, *'kama yeye alivyo, ndivyo tulivyo na sisi ulimwenguni humu.'*

Yohana anatufahamisha kwenye aya ya kumi na nne ya waraka huu wa kwanza sura ya nne kuwa, tunapaswa kupendana kwa sababu 'pendo lililo kamili huitupa nje hofu. Ikiwa unapenda kikamilifu, basi unapaswa kulitupa hofu. Unapoelewa upendo wa Kristo, na hasa maana ya upendo wa Mungu na wa ndugu yako, basi huwa umefahamu jisni kamilifu upendo huo unavyoweza kuondoa hofu. Tunahofia kupoteza maisha yetu na yale tuliyo nayo. Ikiwa tutampenda Mungu kikamilifu, basi tayari tumesalimisha maisha yetu kwake na kila kitu tulicho nacho. Basi ni kipi cha kuhofia?

Kwenye aya ya ishirini, Yohana anazidi kutueleza kuwa tunapaswa kupendana kwani upendo wa juu wa Mungu na ulio sambamba na wa ndugu hazitenganishwi. Mtu anayedai kumpenda Mungu na kumchukia nduguye ni mwogo. Tunapaswa kupendana *kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona.'*

Sababu ya kumi na ni kwa njia ya amri: *'Amri hii tumepewa na yeye, ya kwamba yeye ampendaye Mungu, ampende na ndugu yake.'* Kuna hali ambapo sababu hii ya kumi na Yohana linapaswa kuwa tu lile alilotaka kutupa: Yesu aliamrisha kuwa tupendane.

Kwenye sura ya tano, Yohana anatueleza kuwa imani ni msingi wa hakikisho letu anapoandika kuwa: '*Imani ni ushindi ambao unakabili dunia.'* Tunakabili dunia kwa njia ya imani. Na ikiwa una aina hii ya imani, kuna thibitisho lingine la hakikisho.

Kwenye sura ya tano, Yohana anatueleza kuwa kuna mashahidi watatu katika ushuhuda wetu ambao unatupatia hakikisho. Wakati Yohana anapoelezea juu ya maji, bila shaka anamaanisha ubatiso wa maji. Umuhimu wa ubatiso wa maji ni kuwa unawezesha mtu kuwa mwanafunzi wa siri wa Yesu Kristo.

Waraka Wa Pili Na Wa Tatu Wa Yohana.

Kwenye waraka wa pili na wa tatu wa Yohana, mkazo unatiliwa kwenye ukweli ambao Kristo alifunza. Yohana ni kama mwana thiolojia katika nyaraka hizi mbili kwa sababu anahusika sana na ukweli Yesu aliofunza na msimamo wetu imara kwa ukweli huo. Hana furaha kuu kuliko kuwasikia wanawe wakitembea katika ukweli uliofunzwa na Yesu. Ukweli huo tayari umegeuzwa vibaya wakati Yohana alipoandika nyaraka hizi fupi.

Mtume huyu wa upendo anawashauri wazee ambao anawaandikia kuwa wakali sana kwa watu ambao hawafunzi yale Yesu aliyofunza. Madai, au mafunzo yaliyogeuzwa vibaya ya Yesu Kristo, yalianza zamani katika historia ya Kanisa kwa sababu katika nyaraka hizi fupi utasikia kuwa, '*ikiwa watu hawaamini kuwa Yesu ndiye Kristo, ikiwa hawafunzi katika mtihani wa kanuni, basi usiwaalike kwa maakuli ya mchana. Usiwakatase cho chote. Usiwe na jambo nao.'*

Basi vile Yohana alipokuwa akiandika nyaraka hizi, anazungumzia waraka huu wa pili kwa 'mwanamke mteule.' Ukichukulia maneno hayo kwa hali halisi, basi hiki ndicho tu kitabu katika Biblia yote ambacho kinamzungumzia mwanamke. Kadiri ilivyo, Yohana alikuwa na uhusiano wa uchungaji pamoja na mke huyu mteule.

Lakini alikuwa na shida na watu kama Demetrio ambao, '*wameshuhudiwa na watu wote.*' Nasimulia mtu huyu kwenye aya ya tisa na ya kumi katika waraka wa tatu. Wachungaji siku hizi hupata faraja katika hali kuwa mtume huyu mzee alikuwa na mzee huyu Kanisani mmwake ambaye bila shaka alikuwa kama donda ndugu kwake.

SURA YA KUMI NA NNE.
Waraka Wa Yuda.

Katika waraka huu wa Yuda, utapata kitabu kilicho na sura moja ambacho ni sawa na sura ya pili ya waraka wa pili wa Yohana. Muhimu hapa ya yule anayeandika waraka huu mfupi ni madai au waalimu wa uongo. Mtu kwa jina Yuda aliandika waraka huu. Wasomi husema kuwa mtu huyu alikuwa ndugu mwingine wa Yesu.

Yuda anatufahamisha kuwa alikuwa amepanga kuandika kifungu juu ya wokovu, lakini akabadili wazo lake kwa sababu baadhi ya watu hawakuwa wakihubiri Injili iliyo ya kweli. Wao walikuwa wakihubiri kwa sababu Mungu ni wa neema, Mungu hawenzi kuwarudi wanawe. Yuda alikuwa amehusika sana kuhusu watu ambao walionekana kana kwamba walikuwa wakianguka mbali na imani yao kwa sababu walikuwa wamesikia na kuamini mafunzo hayo.

Yuda anazungumzia juu ya sura ya kumi na nne ya kitabu cha Hesabu, mahali tunaposoma kuwa kizazi chote cha watu wateule wa Mungu walikufa huko jangwani. Walizunguka huko kwa muda wa miaka arobaini kwa sababu hawakuwa na imani ya kuvamia nchi ya Kanaani. Mungu anafanya chaguo mbili. Kalebu na Yoshua ndio walioingia nchi ya Kanaani kwa sababu waliamini na kumfuata Bwana.

Yuda anawakumbusha waalimu wa uongo kuhusu habari za kifo cha kizazi hiki. Waalimu hao wa uongo walikuwa wakiwaambia watu hao kuwa unaweza kufanya jinsi upendavyo na Mungu hatafanya cho chote kuhusu jambo hilo, kana kwamba Mungu mwenyewe alikuwa babu kwao. Maandiko yanatufunza kuwa kuna upande mwingine wa mhusika Mungu- ghadhabu na hukumu- kwa sababu Mungu ni Mtakatifu.

Mfano mwingine Yuda anaowasilisha ni malaika walioanguka. Yuda anaandika kuwa malaika hao walioanguka walitupwa katika shimo lisilo na kina. Mungu hakugonja na kuwatazama malaika ambao hawakuwa wakifanya kulingana na mapenzi yake, bila kuwachukulia hatua yo yote.

Mfano wa tatu wa mwandishi huyu ni Sodoma na Gomora pamoja na miji iliyokuwa kando kando ilivyoangamizwa kwa moto. Yuda anatilia mkazo hukumu la Mungu kupitia mifano hilo anaposhiriki na waalimu hao wa uongo na watu waliokuwa wakiwaamini.

Yuda anatueleza kuwa waalimu hao wa uongo walikuwa kama '*mawimbi ya bahari yasiyozuilika, yakitoa aibu yao wenyewe kama povu.*' Wao walikuwa sawa na '*miti iliyopukutika, isiyo na matunda.*' Tena wao ni kama '*nyota zipoteazo, ambao weusi wa giza ndio akiba yao waliowekewa milele.*' Hatima ya nyota zilizopotea liko sawa na malaika hao walioanguka.

Yuda alikuwa amehusika sana kuhusu wale waliokuwa wametumbukia kwenye lindi la mafunzo hayo ya waalimu wa uongo. Anaandika kuwa tunapaswa kujaribu kurudisha watu hao. Tunapaswa kuwachukua kutoka kwa moto huo bila kuchomeka sisi wenywe. Yuda anamalizia waraka wake kwa baadhi ya mashauri kwa watu waliokuwa

wamerudishwa. Mashauri hayo ni kuhusu kuishi katika kweli ya imani. Napenda mashauri hayo ya mwandishi huyu. Yuda anasema, *'bali ninyi wapenzi, mkijijenga juu ya imani yenu iliyo takatifu sana, na kuomba katika Roho Mtakatifu.'* Kisha anasema, *'jilindeni katika upendo wa Mungu, huku mkingojea rehema ya Bwana wetu Yesu Kristo, hata mpate uzima wa milele.'*

Kwa karne nyingi, wachungaji wametumia dua yake ya kutakia heri kumalizia ibada zao: '*Yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae na kuwasimamisha mbele ya utukufu Wake bila mawaa katika furaha kuu; Yeye aliye Mungu pekee, Mwokozi wetu kwa Yesu Kristo, Bwana wetu; utukufu una yeye, na ukuu, na uwezo, na nguvu, tangu milele, na sasa, na hata milele. Amina* ***(Yuda 24, 25).'***

SURA YA KUMI NA TANO
Kitabu Cha Ufunuo Wa Yohana.

Kwenye aya za utangulizi za kitabu hiki cha Ufunuo waYohana, tunasoma kuwa mtume Yohana alikuwa kwenye kisiwa cha Patmo kwa sababu ya imani yake. Ukilinganisha Maandiko kwa historia, tunaazimia kuwa Yohana alikuwa uhamishoni kwenye kisiwa hicho kikavu. Wasomi hawakubalini kuhusu kama alikuwa huko peke yake au alikuwa huko kama mtumishi mfungwa. Akikuwa huko, alishuhudia ufunuo wa Yesu Kristo. Neno 'ufunuo' hutokana na Neno la Kiyunani, 'funuo' maanake 'kuvuta nyuma pazia.'

Lugha Ya Ishara Ya Mwokozi

Ufunuo huu 'ulidhihirishwa kwa Yohana,' kumaanisha kuwa ulipeanwa kwake kwa hali ya 'lugha ya ishara.' Wayahudi walikuwa na lugha ya ishara' nzuri sana ya Biblia na tunaona kuwa lugha hiyo ya ishara ikidhihirishwa hapa katika kitabu cha Ufunuo. Utakumbuka kuwa neno 'ishara' ni moja ya maneno mazuri sana ya Yohana ***(Yohana 20:30, 31; 2:11; 21:25).*** Katika kitabu hiki, ishara hizo ni za Kibiblia. Utazipata mahali kwingine katika Biblia na bila shaka kuzielewa; jambo ambalo litakuwezesha kuelewa kitabu cha Ufunuo.

Unapokisoma kitabu cha Ufunuo, fanya ramani yako mwenyewe. Kwa kuwa utahitaji kurasa nyingi kwenye ramani hiyo, ningekushauri uwe na kijitabu kikubwa ambacho kina kurasa nyingi. Chora mistari ya kwenda juu kwenye ramani hii kwa hali ya kufanya vijisehemu. Katika sehemu ya kwanza ya ramani hii, andika neno 'ishara.' Orodhesha ishara ambazo zinapatikana kwenye kitabu hiki katika sehemu hiyo ya kwanza- kwa mfano: Farasi mweupe, bahari ya kioo, wanyama wanne, vinara saba vya mishumaa na kadhalika.

Kwenye sehemu ya pili, weka hapo juu maneno haya, 'Ufunuo wa kibinafsi.' Mwulize Roho Mtakatifu avute nyuma pazia na kukuonyesha maana ya ishara hizo. Weka maana hayo kwenye sehemu hiyo ya kibinafsi.

Hapo juu ya sehemu ya tatu andika: Maelezo ya Biblia,' kisha uorodheshe mahali kila ishara inapopatikana kwenye Biblia. Ikiwa unaweza kupata maelezo mazuri, kwenye sehemu ile nyingine andika kile kila ishara inachofunza.

Kisha, kwenye sehemu ya mwisho ya ramani hii, weka maelezo hayo ya mwisho. Ukifanya kazi hiyo kabisa, basi utakuwa na ramani yenye kurasa mia moja hamsini za kitabu cha Ufunuo wa Yohana.

Funguo Zinazifungua Kitabu Cha Ufunuo

Unapitia lugha hii ya ishara ya kitabu cha Ufunuo kilipeanwa kwa Yohana, utatambua, kuwa ni kana kwamba kiliandikwa kutoka kwa Mungu hadi kwa watu wake kwa taratibu. Basi unapojaribu kufungua ujumbe huo wa taratibu, ili kuelewa ujumbe wenywe, unapaswa kuwa na ufunguo wa kufungua taratibu zenyewe.

UFUNGUO WA KWANZA

Ufunguo wa kwanza ni Roho Mtakatifu. Huwezi kuelewa mambo ya kiroho bila Roho Mtakatifu. Haya ni kweli hasa unapoingia kwenye kitabu hiki cha Ufunuo wa Yohana. Yesu aliwaambia mitume kuwa alikuwa akiwapa Roho Mtakatifu, ambaye alimtaja kama Mfariji, na kuwa angewajulisha kuhusu mambo yatakayokuja.

UFUNGUO WA PILI

Ufunguo wa pili wa ujumbe huu wa taratibu ni kuwa, ishara hizo ni za Kibiblia. Ikiwa wewe ni Myahudi, ambaye unafahamu sana Agano Jipya, basi ishara hizi sio geni kwako. Kwa mfano, katika sura ya nne, mlango unafunguka mbinguni kisha unaona mtu ameketi kwenye kiti cha enzi. Anaonekana mithili ya jiwe la yaspi na akiki, na upinde wa mvua ulikizunguka kile kiti cha enzi, ukionekana mithili ya zumaridi.

Myahudi angefahamu kuwa katika kitabu cha Kutoka sura ya ishirini na nane, kuhani mkuu alikuwa akivalia kifuko cha kifuani ambazo kilikuwa kimetiwa mawe ambayo kila moja lilikuwa likiwakilisha kabila zote kumi na mbili za Israeli. Jiwe la kwanza lilikuwa akiki. Jiwe hilo liliwakilisha kabila la zamani la Israeli-kabila la Reubeni. Nayo jiwe la mwisho lilikuwa yaspi ambalo liliwakilisha jamii la Benyamini. Zumaridi ndio lililokuwa jiwe la saba ambalo liliwakilisha jamii ya Yuda. Kwa lugha ya kiebrania, majina hayo yalikuwa na maana fulani. Reubeni lilimaanisha ‘Tazama, Mwana wangu!’ Benyamini maanake ni, ‘Mwana wa mkono wangu wa kuume’, kisha Yuda humaanisha ‘tukuza.’ Kwa hivyo, kile tulicho nacho hapa katika lugha ya ishara ndio hiki: Unapotazama katika mlango wa mbinguni, kuna kiti cha enzi na aliyeketi kwenye kiti chenyewe anaelezewa na mawe hayo ambayo yana ujumbe, ‘Tazama, Mwanangu, Mwana wa mkono wangu wa kuume! Mtukuze!’

Kuna msemo ambao unapatikana mara nyingi katika kitabu cha mwisho cha Biblia: Mimi ni Alfa na Omega.’ Neno la kwanza katika sarufi za Kiyunani ni alfa ilhali ya mwisho ni omega. Hizi huwa zinatafsiriwa kumaanisha, ‘Mimi ni wa kwanza na wa mwisho.’ Tutaenda kuwa na ufunuo wa Mmoja, Yesu Kristo; ambaye Mwenyewe siye mwanzo na mwisho

Kuabudu Kwa Milele

Katika sura ya nne na ya tano, tuna fursa nzuri ya wokovu ambayo inatendeka katika hali ya umilele. Jambo nzuri linatendeka hapa. Mungu Baba anaamurisha kusujudu kwa mbinguni kuondolewa kwake hadi kwa mwanawe, Mwana kondoo, ambaye ni kana kwamba amechinjwa. Mungu anasema hapa, *‘Msujudu Mwanangu. Mwabudu*

Mwanangu kwa sababu ya vile alivyo, kwa hali ya kile alicho, na kile atawahi kuwa, msujudu Mwanangu!'

Kwa kuwa ishara hizi ni za kibiblia, unaweza kuona kwa nini watu hawa walitayarisha kitabu hiki cha Biblia na kukiweka huko mwisho. Kusudi la kufahamu kitabu cha Ufunuo, ambacho ndio cha mwisho katika Biblia, ni kuelewa vitabu vile vingine sitini na tano vya Biblia.

Kuna baadhi ya ishara zingine za Biblia. Ningetaka kutumia kielezo katika ufunguo huu muhimu. Tambua kwa mfano katika kitabu hiki cha ***Ufunuo 1:4, 4:5 na 5:6,*** kumetajwa 'roho saba wa Mungu.'

Watu wanaotilia umuhimu mwingi katika idadia u takwimu katika Maandiko wanatufahamisha kuwa nambari saba ni ya ukamilifu, au kutimika. Jambo hili linadokeza kuwa roho saba wa Mungu wanawakilisha roho ya Mungu kamilifu, iliyotosha. Katika kusudi lake, Mungu ni wa kiroho. Hata hivyo, wasomi wengi wanaamini kuwa dhana la 'roho saba wa Mungu,' inaturudisha nyuma kwenye unabii wa Isaya.

Katika unabii wa Isaya, mwana mfalme wa manabii alitupa unabii wa Kimasihi ambao unaelezea roho saba wa Mungu. Unabii wa Isaya unatimizwa katika ufunuo uliotolewa kwa mtume Yohana kuhusu roho saba wa Mungu. Isaya aliandika hivi: '*basi nalitoka chipukizi katika shina la Yese, na tawi litakalotoka katika mizizi yake litazaa matunda. Na roho ya Bwana atakaa juu yake, roho ya hekima na ufahamu, roho ya shauri na uweza, roho ya maarifa na ya kumcha Bwana.'* Katika aya ifuatayo, Isaya anazidi kusema kuwa furaha yake itakuwa katika kumcha Bwana ***(Isaya 11:1,2,3).'***

Isaya anatueleza kuwa wakati Masihi atakapokuja, Yesu Kristo atakuwa dhihirisho kamili la Mungu, ambaye asili yake ni roho. Kulingana na Isaya, Yesu Kristo bali na kudhihirisha asili hili la Roho saba za Mungu, pia kwenye saburi lake atadhihirisha uzima ambao kweli umejazwa na kuongozwa na Roho. Yohana anatufahamisha kuwa unabii wa Isaya ulitimizwa wakati Yesu alipokuja.

Tunaona vinara saba vya taa ambavyo vimesimama kando na kiti cha enzi. Tunafahamishwa kuwa taa hizo saba zinawakilisha Roho saba wa Mungu. Kisha tunazidi kusoma, *'nikaona katika kile kiti cha enzi na wale wenye uhai wanne, na katikati ya wale wazee, Mwana-Kondoo amesimama, alikuwa kana kwamba amechinjwa, mwenye pembe saba na macho saba, ambazo ni Roho saba za Mungu zilizotumwa katika dunia yote* (***5:6).'***

Wasomi wanaamini kuwa pembe zinawakilisha nguvu ilhali macho yanawakilisha hekima katika Maandiko. Kwa hivyo, mwana Kondoo huyu ambaye alikaa kana kwamba amechinjwa, ni kielelezo cha roho saba wa Mungu. Na kielelezo hiki cha roho saba wa Mungu pia ni kielelezo mwafaka cha nguvu na hekima ya Mungu wakati alipochinjwa.

Roho ya Bwana lilikuwa muhimu sana katika huduma ya Yesu. Yesu alikuwa na roho ya <u>hekima,</u> kumaanisha alikuwa na roho ya hekima, hekima kamilifu ya neno la Mungu. Pia alikuwa na Roho ya <u>ufahamu,</u> kumaanisha aliwakuwa na ufahamu kamilifu wa neno na mapenzi ya Babake.

Yesu alikuwa na Roho ya <u>maarifa</u> kwa sababu aliishi kikamilifu katika Neno la Mungu, na kuwafunza wale wengine jinsi ya kujumulisha Neno la Mungu. Kisha, Roho ya <u>shauri</u> ni sehemu ya kielelezo mwafaka cha Roho ya Mungu. Vile Yesu alivyoshiriki nasi Neno la Mungu na matumizi yake katika maisha ya watu aliowahoji, alikuwa akidhihirisha Roho ya shauri. Aliposhikiri Neno la Mungu pamoja na watu, kisha nao

wakalijumulisha katika maisha yao, Roho Mtakatifu alitia mafuta Neno kwa nguvu zaidi. Hapa ndio wakati Roho ya uweza linapodhihirishwa kupitia Yesu.

Kisha, Roho ya kuabudu lilikuwa wazi sana katika maisha ya Yesu. Isaya anatueleza kuwa furaha yake ni katika Roho ya kuabudu. Unaposoma Injili zote nne, utaona kuwa wakati Yesu alipokuwa hawahudumii watu, Alikuwa peke yake usiku kucha, au alikuwa akiamka alfajiri na mapema na kuanza kumwabudu Baba yake

Mlango Ukafunguka Mbinguni

Kwenye sura ya nne, aya ya kwanza, tunasoma kuwa wakati Yohana alipopokea mwaliko wa, *'panda hata huku, nami nitakuonyesha mambo ambayo hayana budi kuwako baada ya hayo,'* ilikuwa sauti ya baragumu ambalo lilimwalika katika ufunuo huu wa mbinguni. Baadhi ya wayu waamini kuwa hili ni ishara ya Biblia ambalo linaelezea juu ya kunyakuliwa kwa Kanisa. Mtume Paulo anaandika kuwa kunyakuliwa kwa Kanisa tunatangazwa kupitia sauti ya baragumu. (***1 Wathesalonike 4:16; 1Wakorintho 15:52).'***

Wakati Yohana anapotazama kwenye mlango huu wa mbinguni, anaona kiti cha enzi ambacho ni ishara kuu ya mbinguni. Mbele ya kiti hicho cha mbinguni, Yohana anaona bahari la kioo. Katika hema la kuabudu na hekalu la Sulemani, kuna birika ambalo Kuhani alikuwa akijitakasa kabla ya kujitokeza na kuwatetea watu mbele za Mungu. Ujumbe ulikuwa kwamba, tunapaswa kujitakaza kabla ya kujitokeza mbele za Mungu. Kuhani walikuwa kila mara wakirudia ukaribio huu kwa Mungu kwa niaba ya wenye dhambi kwa sababu watu hao kila mara walihitaji msamaha. Katika bahari la kioo ambalo lilikuwa mbele ya kiti cha enzi, maji yaliganda na kuwa barafu, ambalo liliwakilisha utakaso wa kudumu wa milele.

Katika sura ya tano, kuna kitabu ambacho kina mihuri saba na wote waliokuwa huko mbinguni hawangeweza kuvunja mihuri hiyo. Hakuna mtu aliyeweza au kustahili kuvunjwa mihuri hiyo. Ishara hili la Biblia linaturudisha nyuma kwenye kitabu cha Ruthu na dhana ya mkombozi wa jamii. Wakati mtu kama Boazi alipotaka kumkomboa Ruthu, deni za mwana mke huyo zilitiwa muhuri katika chuo. Hakuruhusiwa kuvunja mihuri hiyo na kutazama kilichokuwa ndani ya chuo hicho hadi alipodhihirisha nia yake ya kumkomboa.

Ujumbe wa tukio hili la mbinguni ni kuwa mbingu limejaa watu ambao wanataka kukombolewa, lakini hakuna mtu aliye na uwezo wa kuwakomboa. Yohana alitoa machozi kwa sababu hakukuwa na Mkombozi. Kisha, tunasikia habari njema, *'Usilie; tazama, Simba aliye wa kabila ya Yuda, Shina la Daudi, yeye ameshinda apate kukifungua kile kitabu, na zile mihuri zake saba **(5:5).'***

Wakati mlango ulipofunguka huko mbinguni, tunasoma kuwa kuna viti vingine ishirini vya enzi kuzunguka kiti kikuu cha enzi, na kwenye viti hivi, wameketi wazee ishirini. Wazee hawa wanawakilisha uongozi wa watu wa Mungu- labda makabila kumi na mawili ya Israeli na mitume kumi na wawili.

UFUNGUO WA TATU

Ufunguo wa tatu, ambao unatusaidia kuvunja taratibu za ujumbe huu kutoka kwa Mungu, ni kazi ambalo lilipeanwa kwa Yohana. Kazi hilo linafanya, utaratibu wa Ufunuo ambao ulipokelewa na Yohana akiwa kisiwani huko Patmo. Sura ya kwanza, aya ya kumi

na tisa, inatupatia kazi hilo na utaratibu wake. Yohana aliamrishwa kuwa '*haya uyaonayo uyaandike katika chuo, na yale yatakayotendeka baada ya haya.'*

Kwenye sura ya kwanza ya kitabu hiki, tunasoma kuhusu ushuhuda huo wa Yohana. Kile Yohana alichoona katika sura hili la kwanza kinaelezea sehemu ya kwanza ya kazi yake alipoambiwa, '*uyaandike mambo hayo uyaonayo akayapeleke kwa hayo Makanisa sana yaliyokuwa huko Asia Minor kwa wakati huo*.

Yohana aligeuka kutazama sawa na jinsi Musa alipogeuka kumwoma Mungu katika kijiti kilichokuwa kikiwaka huko jangwani. ***(Kutoka 3:3,4).*** Yohana aligeuka kuona sauti iliyokuwa ikimzungumzia. Tambua viarifa ambavyo Yohana anatumia anaposimulia ushuhuda wake kwetu. 'Na nilipogeuka,' anasema kuwa, 'niliona.' Nami nilipomwona, naliaguka miguuni pake kama mtu aliyekufa.' Maanake ni kwamba, sharti la kumshuhudia Mungu kwanza ni kugeuka.

Mtume Yohana alikuwa akimalizia sehemu yake ya kwanza ya kazi yake aliporekodi ushuhuda huo. Baada ya Yohana kujulishwa, 'kuyaandika mambo hayo aliyoyaona,' kisha aliamrishwa, 'uyaandike mambo hayo yalivyo.' Yohana alimaliza sehemu yake ya pili katika sura ya pili na ya tatu wakati alipoandika nyaraka hizo kwa Makanisa ya huko *Asia Minor.*

Kwa muhtasari, sura ya kwanza inalingana na mambo ambayo Yohana aliona wakati aliposhuhudia hayo. Sura ya pili na ya tatu ndio sehemu ya pili ya kazi yake, ambalo lilikuwa, 'uyaandike hayo yalivyo,' yaani, mambo yale yaliyokuwa katika Makanisa hayo saba. Makanisa hayo yalikuwa Efeso, Smirna, Pergamo, Thiatira, Sardi na Filadelfia na Laodikia ambayo yalikuwa Makanisa ya kweli.

Kumbuka kuwa katika sura ya kwanza ya kitabu hiki, Yohana aliona vinara saba vya taa? Ufunuo wake wa Kristo ulikuwa kwamba Kristo alikuwa katikati mwa vinara hivyo vya taa. Yohana alisema kuwa aliyekuwa katikati mwa vinara hivyo vya taa alikuwa ni Kristo. Ingawa Makanisa hayo yalikuwa na shida nyingi kweli, Kristo aliyefufuka, aishiye yuko katikati mwake. Haijalishi yamepungukiwa na nini, usiwahi kusahau kuwa: Kristo alikuwa katikati mwa Makanisa Yake.

Waraka kwa Kanisa la Efeso ulikuwa ukisema hivi: '*umeuacha upendo wako*.' Jambo hilo linanishangaza sana kwa sababu Timotheo alikuwa kiongozi wa Kanisa hilo. Paulo aliliambia Kanisa la Filipi kuwa alikuwa anamtuma Timotheo kwao kwa sababu hakuwa anajua mtu mwingine ambaye alikuwa na upendo sawa na Timotheo. Alikuwa anawajali wengine. Sasa, inaonekana kana kwamba waraka huu kwa Kanisa lililokuwa chini ya uongozi wa Timotheo linaulizwa na Kristo aliyefufuka, 'je, ni nini lililotendeka kwa upendo wenu?' Ikiwa unajihisi kuwa u mtu ambaye kupitia kwake, Bwana anawapenda watu wake, usiwahi kusahau kuwa unaweza kupoteza ushuhuda huo wako wa kuwa chombo ambacho kupitia kwake, Kristo anawapenda watu ambao amekupatia kwa pendo Lake.

UFUNGUO WA NNE

Sehemu kubwa ya kazi iliyopewa Yohana hapo mwanzo wa sura ya nne ni: '*uyaandike mambo ambayo hayana budi kuwako baada ya hayo.'* Kitabu chote cha Ufunuo kinahsu mambo ambayo hayana budi kuwako siku za usoni.

Kutazamia ufunguo huo wa nne, unapaswa kuelewa utaratibu wa kuanzia sura ya sita hadi ya kumi na sita katika kitabu hiki. Sura ya nne na ya tano ni lugha ya ishara nzuri sana ambayo inasimulia kuabudu ambako kutatokea huku mbinguni. Lakini

unapoingia kwenye sura ya sita ya kitabu hiki, mambo yanabadilika na kuwa magumu kuelewa.

Mfululizo wa matukio ambayo yanajulikana kama Mjio wa pili wa Yesu Kristo yanachukua kipindi kirefu sana. Mengi ya matukio yaliyozungumziwa kutoka tukio la kwanza hadi la mwisho tayari yamefanyika. Hakika ya muda inatengemea jinsi unavyotafsiri matukio hayo na jinsi ya kuyapanga kwa utaratibu. Moja ya matukio mafupi sana ni kipindi cha miaka saba ambacho kinajulikana kama 'Dhiki Kuu.' Yesu anasimulia hayo kwenye maongozi yake mlimani wa Mizeituni kwenye ***(Mathayo 24: 21-29).***

Wasomi wengi wanaamini kuwa Dhiki Kuu litakuwa kwa muda wa kipindi cha miaka saba. Dhiki hii kuu ni kile sura za sita hadi kumi na tisa zinachosimulia. Sura hizi zote, kutoka sura ya sita, wakati farasi hao walipojitokeza hadi katikati mwa sura ya kumi na tisa, zinazungumzia juu ya kipindi kimoja kifupi sana cha miaka saba kati ya matukio ambayo yanajulikana kama 'Kuja kwa mara ya pili kwa Yesu Kristo.'

Dhiki Kuu inasimuliwa katika sehemu hii ya kitabu cha Ufunuo kama matukio ya hukumu. Unaposoma ufunuo huu wa Yohana, mihuri saba imevunjwa. Kila mara muhuri unapovunjwa, kunatokea hukumu kali na ya kutisha! Kisha unasoma kuhusu baragumu saba. Kila mara baragumu hizo saba zinapopigwa, kunafanyika hukumu ya kutisha.

Mihuri inavunjwa katika sura ya sita, baragumu zinapigwa kwenye sura za nane na tisa. Kisha, kwenye sura ya kumi na sita, unasoma kuhusu vitasa saba. Vitasa hivyo vinamiminiwa na kila mara vinapomiminiwa, hukumu inafanyika.

Baadhi ya hukumu hizo za mihuri, baragumu na vitasa, ni za mfululizo. Wengine huamini kuwa kipindi kimoja cha hukumu kinasimuliwa kwa njia tatu tofauti. Kati ya hukumu hizo tatu, kuna maelezo ambayo, kadiri ilivyo, yameongezewa kwenye maelezo kuhusu hukumu. Hata hivyo, maelezo hayo, kwenye sura ya tisa, kumi hadi ya kumi na tano, na kumi na saba hadi kumi na tisa, bila shaka sio katika utaratibu mwafaka.

UFUNGUO WA TANO

Ufunguo wa tano ambao unafungua ujumbe huu kwenye kitabu cha Ufunuo unafahamika kama: <u>Kuwa na saburi kuhusu utaratibu huu wa matukio yote</u> ambayo yanazungumiwa kwenye kitabu cha Ufunuo. Nina subira sana kuhusu uwezekano wa utaratibu huo ninaodokeza. Kulingana na Yesu, hakuna mtu anayejua siku wala saa wakati mwisho utakapofika- sio malaika, wala sio mwana wa Mungu mwenyewe. Ni Baba tu anajuaye. (***Mathayo 24: 36)*** Wakati mitume na wanafunzi wa zamani walipomwuliza Yesu habari za mambo ya kudumisha ufalme wa Israeli, alijibu kuwa sio kwa ajili yao kujua saa wala majira ya matukio hayo kwa sababu Baba aliamua kuyaweka kwake binafsi **(*Matendo ya Mitume 1: 7*).**' Sasa, nisaidie, ikiwaamalaika hawajui, Mwana wa Mungu hajui, ikiwa ni Baba peke yake anayejua, je tunawezaje kuwa vingine bali na kuwa wenye subira tunapojaribu kuweka kwa pamoja utaratibu wa 'nyakati na majira' ya matukio hayo?

Moja ya matukio hayo ni kunyakuliwa kwa Kanisa. Baada ya Kanisa kuchukuliwa kutoka hapa duniani, tunaweza kutarajia Dhiki Kuu. Kisha, kuna kurudi kwa mara ya pili kwa Kristo. Atakaporudi, sio kuchukua Kanisa lake hapa, bali kurudi nayo hapa kutawala. Baadhi ya watu huamini kuwa kutawala huko kutakuwa ufalme halisi ambao utadumu kwa miaka elfu moja. Ilhali wengine yamegawanyika kati vile wanavyoweza kutafsiri matukio hao. Haijalishi ni jinsi gani unavyotafsiri matukio hayo,

wengi hawatakubaliana nawe. Kuwa mwenye subira kuhusu utaratibu wako na tafsiri lako la matukio haya.

UFUNGUO WA SITA

Nia yetu katika kusoma kitabu hiki cha Ufunuo linapaswa kuwa kuabudu au kusujudu, kuliko kufahamu. Hili ni muhimu sana. Baraka zimeahidiwa juu ya yule atakakaye soma kitabu hiki na kuyashuhudia (***22:18).*** Kuna kweli nyingi katika kitabu hiki-hasa kwenye nyaraka kwa Makanisa-ambayo ni ya maelezo na Injili. Kuna kweli nyingi katika kitabu cha Ufunuo ambazo tunaelezwa na kushauriwa kutii. Waumini wana tabia ya kusujudu ufahamu wa kitabu hiki badala ya Mungu na Kristo aliyefufuka aliyempa Yohana kitabu chenyewe.

Mtume huyu mpendwa anaelezea ufunguo huu nyakati mbili hapo mwisho wa kitabu hiki. Tunasoma kuwa Yohana alianguka miguuni pa malaika aliyetafisiri ishara hizo zote kwake na kumsujudu. Tunaweza kufahamu kwa nini alipaswa, lakini malaika huyo alisema, '*Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu. Msujudie Mungu. Kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio roho na unabii **(19:10, 22:8)***

Huyu ni ujumbe mwafaka wa nia ya kusoma kitabu hiki. Nia hiyo sio tu kuelewa yote, bali ni kusoma kitabu hiki cha Ufunuo sawa na jinsi unavyosoma Injili ya Yohana-kumwona Yesu. Kisha msujudu Yesu unayemwona, na umwabudu Mungu! Wacha kitabu hiki kiongeze hali yako ya kutisha, kustaajabu na kuabudu. Unaposoma kitabu hiki, nenda mbele za Uwepo wa Mungu.

UFUNGUO WA SABA

Ufunguo wa saba ni kuuliza swali, 'kwa nini Mungu alitueleza mambo hayo kuhusu nyakati za usoni?' Jinsi tumeona mara nyingi hapo awali, wakati Mungu anapovuta nyuma pazia na kutueleza jambo kuhusu jinsi inatakavyokuwa hapo mwisho, ana nia ya kuvuta nyuma pazia hiyo.

Matumizi yanaonekana kuwa: 'Kwa sababu ya haki kwamba nimewaonyesha nyuma ya pazia yale yatakayofanyika, ni aina gani ya watu tunaopaswa kuwa sasa hivi katika hali hii? Ni maisha gani takatifu tunaopaswa kuwa tunaishi!'Mungu anataka tuishi maisha yetu ya sasa, ya kila siku kwa hali ya mambo yote ambayo ametufunulia katika kitabu hiki cha Biblia.

UFUNGUO WA NANE

Jiadhari na mawazo tamanifu unapotazama nyuma ya pazia na kuona yale yatakayotendeka kulingana na hali ya umilele. Maandiko yanatueleza kuhusu maisha baada ya kaburi kwa kutumia ishara. Wengi hutafsiri aina hii ya Maandiko jinsi wanavyotaka hali hiyo iwe. Ukweli wa ufunuo huu hautengemei mawazo tamanifu. Ikiwa kweli unataka kujua kuhusu maisha baada ya dunia hii kupita na kaburi, basi ni sharti usome kitabu hiki ukiwa na mawazo yaliyo wazi.

UFUNGUO WA TISA

Tunapata ufunguo wa tisa kwenye sura ya nne na ya tano. Unapopitia kwenye mlango ulio wazi hadi mbinguni, tambua kuwa kila ishara iliyotajwa katika sura hizi nzuri sana inaelezwa kulingana na mahali pake kwenye kiti cha enzi ambacho ndio kikuu

huku mbinguni. Mwana-Kondoo amesimama katikati mwa kiti cha Enzi. Viti vile vingine ishirini na vinne vya enzi vinazunguka kiti hiki kikuu. Sauti ya gurumo na umeme zinatokea kwenye kiti hicho. Taa saba za moto ziko mbele ya kiti; mfano wa bahari ya kioo, kama bilauri liko mbele ya kiti. Sauti ya malaika wengi inasikika kando mwa kiti hicho cha enzi.

Kwenye sura ya nne na tano, unapata watakatifu ambao wamekizunguka kiti cha enzi cha Mungu waakimba wimbo mpya. Hili ni nzuri sana! Hata hivyo, kuna wenye dhambi ambao wanasujudu Mwana Kondoo ambaye yuko kwenye kiti hicho cha enzi, lakini hawana mahali pao kwenye kiti hicho. Unapaswa kuazimia kuwa wenye dhambi ambao wanasujudu Mwana- Kondoo ni kutoka kuzimu kwa sababu hawatoki mbinguni. Jambo hilo ni la kutisha!

UFUNGUO WA KUMI

Tambua katika kitabu cha Ufunuo kuna michezo miwili inayosimuliwa kwa wakati mmoja. Mchezo wa mbinguni ambao unasimuliwa kwenye sura za nne, tano, sita kumi na kenda, ishirini, ishirini na moja na ishirini na mbili, kisha kwa wakati huo pia kuna mchezo wa kidunia ambao unasimuliwa kwenye sura ya sita, nane, tisa, kumi na sita, kumi na tisa na ishirini. Sura ya kumi na tisa na ishirini zinagawanyika katikati jinsi zinavyosimulia michezo yote miwili.

UFUNGUO WA KUMI NA MOJA

Huu ndio ufunuo wa Yesu Kristo, sio kitabu cha Ufunuo. Kuanzia sura ya kwanza hadi ya ishirini na mbili, hili ni moja ya ufunuo unaoendelea wa Yesu Kristo. Sawa na vile ulivyotazamia Yesu Kristo katika Injili ya Yohana na kwenye agano la kale, mtazamie hivyo katika kitabu cha Ufunuo. Tazama jinsi Yesu anavyofunuliwa kama mfalme kamili wa wafalme na Bwana wa mabwana.

UFUNGUO WA KUMI NA MBILI

Yohana alifahamishwa kuwa angekuwa na ufunuo wa mambo ambayo hayana budi kuwako baada ya hayo ***(4:1***). Kwa kuwa Mwenyezi Mungu ni Mungu wa haki, na kuna ukosefu wa haki sana hapa duniani, unapaswa kuwa na hali kamilifu sawa na hukumu zinazosimuliwa katika kitabu cha Ufunuo ambao ulipeanwa kwa mtume Yohana.

UFUNGUO WA KUMI NA TATU

Ingawa tunapaswa kusoma ili kusujudu bali na kufahamu, soma ufunuo huu ukitambua kuwa kuna mengi ya kufahamu. Baraka zinaahidiwa ikiwa utasoma kitabu hiki kweli ukisikia ujumbe wake kisha kuujumulishwa katika maisha yako (**22: 18).**

UFUNGUO WA KUMI NA NNE

Punde unaposoma kitabu hiki cha mwisho katika Biblia, kulinganishe na vitabu vile vingine, na vingine vya Maandiko ambavyo vinatujulisha kuhusu mambo ya mwisho. Vifungu hivi vyote vya Maandiko, tangu manabii hadi mafunzo ya Yesu na ya mitume, yanakupa changa moto kwa swali hili: ‘je yale uliyoyasoma kuhusu asili kamili ya mambo yatakayokuja, yamehusika na yale unayoamini, thamani zako vile unavyoishi maisha yako leo?’

Tunajifunza kutokana na kifungu hiki cha Ufunuo kuwa watakatifu wanaoimba wimbo mpya kwenye kiti cha enzi watakuwa kutoka kwa kila kabila na lugha na jamii na kila taifa (***5:9).*** Unapofikiri kuhusu jinsi walivyofika hapo je, hali hiyo inashawishi vipi mtazamo wako kuhusu Agizo Kuu la Yesu Kristo na kazi ya Bwana ambaye anajenga Kanisa lake kote duniani?

Neno la Mungu linaanza kwa Mungu akiuliza binadamu swali hili, 'Uko wapi?' Biblia inamalizikia kwa swali lingine la kutisha: 'Utakuwa wapi wakati matukio hayo yote yanayosimuliwa katika kitabu hiki cha kutisha yatakapotimia? Kweli kuna mambo mawili yanayowekana. Aidha utakuwa huko mbinguni pamoja na watakatifu mkiimba mbele ya kiti cha enzi au utakuwa pamoja na wenye dhambi ukimsijudu Mwana-Kondoo kutoka kuzimu. Mahali utakapokuwa wakati huo panatengemea mahali ulipo kwa sasa katika msimamo wako kwa Injili ya Yesu Kristo.

Kote katika karne ya historia ya Kanisa, mamilioni ya watu wameongozwa na imani kusoma kitabu hiki cha mwisho katika Biblia. Ombi langu ni kuwa, ikiwa haujamwamini Yesu Kristo kuwa Mwokozi na kumtawaza kuwa Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, basi uchunguzi huu mfupi wa kitabu cha Ufunuo utakuongoza kuazimia kuhusu kiwango cha umilele chako.